

# *KWA NINI NINACHUKIA*

## *DINI ZA KIMADHEHEBU*

Asante, Ndugu Neville. Mwaweza kuketi. Kwanza, nimekuwa na shughuli nyingi sana leo mpaka nimekosa kuchukua simu za wagonjwa. Kulikuwa na baadhi ya watu waliokuwa wakingojea mazungumzo ya kibinafsi ya kuombewa, ambao nilipaswa kuonana nao. Lakini sasa baadhi ya . . . mmoja wao, ninaamini Billy alisema alitoka Canada, sehemu mbili ama tatu mbalimbali. Sasa, wao wanawasili hapa, unajua, na kukaa hotelini na kwenye maloji kila mara. Nami huenda kuonana nao, kukutana nao na kuwaombea wakija kutoka pande zote ulimwenguni, na Asia, Ulaya na kila mahali. Kila siku, wakati tukiwa hapa, watu wanakuja. Kuna zaidi ya mia sita kwenye orodha, wakingojea mazungumzo ya faragha, na kwa hiyo inakuwa ni jambo ligumu. Lakini watu walio wagonjwa sana na wa kuombewa, mbona, mimi hujitahidi kuonana nao.

<sup>2</sup> Ninii tu, vema, kwa kuwa nimekuwa kule ndani pamoja na halmashauri yangu ya wadhamini, juu ya mazungumzo madogo pamoja na halmashauri yangu ya wadhamini hapa kanisani, ilitubidi tuonane muda mfupi uliopita. Na katika wakati huo nikachelewa kama saa moja na nusu, na kulikuwako na baadhi ya watu waliopaswa kuwa hapa wakati huo ili kuombewa. Kama wapo hapa, ningetaka kuwaombea wakati huu. Kwa hiyo, tafadhalini, wale watu waliopaswa kuombewa, vema, wanaombwa kuja tu hapa sasa wakati mpiga piano, ye yote yule, atakuja na—na kutupa sauti kidogo ya “Ni Tabibu wa karibu, tabibu wa ajabu.” Sasa wale watakaoombewa, kama wakiweza, kwamba walikuwa ni wangapi sijui. Na ninyi ndio wale ndugu, nadhani. Ndugu, mimi nimeteseka sana katika mwili wangu mwenyewe. Yesu alichukua katika mwili Wake, maumivu makali, apate kuwa Mpatanishi anayefaa, kwa sababu Yeye alikuwa Mungu aliyefanya mwili apate kuteseka. Yeye angeweza kusikia uchungu wa magonjwa. Na hiyo ndiyo sababu Yeye alikuja kufanya upatanisho. Na katika jambo hili Yeye akaliagiza Kanisa Lake liendeleze kazi Yake.

<sup>3</sup> Nami nimeninii—ninahehimu sana kazi ya madaktari, upasuaji na kadhalika, ambao—ambao kwa majaliwa yao ambayo Mungu amewatunukia kufanya mwili mambo fulani, kufanya upasuaji na kung’oa meno ambayo yameharibika, na kadhalika. Ninathamini jambo hilo. Lakini unafikia wakati ambapo yana—yanawashinda, ha—hawajui la kufanya. Unaona? Nami nafikiri, basi, tuna haki kamilifu, kama ambavyo tungalikuwa nayo katika mambo ya kawaida, kama

tungalimwendea daktari wa familia yetu, labda da—daktari huko mashambani, maskini mzee daktari fulani anayebeba taa ya mkono na kupita mbugani usiku, kukutafuta, kukutibu. Na akishindwa kujua, yeye atamwendea mtu fulani aliye mjuzi zaidi kuliko yeye. Atakupeleka kwa mtaalamu. Na sasa kama mtaalamu hajui, ni—nina furaha tuna kimbilio lingine, yule Tabibu mkuu.

<sup>4</sup> Na Yeye hashindwi, Huyu hashindwi, kwa sababu Yeye Mwenyewe ndiye Muumba. Naye ametufanya njia. Sasa, kama kungali kwako na nguvu za uponyaji zo zote ndani yangu kufanya jambo hilo, ni—ningekuja kule na kufanya hivyo. Ni—ningefurahia tu kufanya jambo hilo. Lakini, kuhusu nguvu za uponyaji, mimi sina, hakuna mtu mwingine aliye na nguvu za uponyaji. Lakini tumeagizwa, unaona, kutoka kwa Kristo, kuwaombea wagonjwa, Ambaye tayari ameweka akiba nguvu za uponyaji. Unaona? Nasi tunakuja tu, tuseme, kuandika hundi yake. “Na lo lote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu,” hiyo ni hundi iliyowazi, “lo lote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, hilo nitalifanya.” Ni ahadi ya jinsi gani! Hakika haiwezi kushindwa. Nami nimewasaidia ndugu zangu na dada zangu, kote ulimwenguni, waweke akiba hizi... ama wachukue mambo haya kwenye Benki ya Mungu, kwa Damu ya Yesu Kristo. Na jambo hilo limefanikiwa sana. Yeye daima amelipia, na kwa sababu hiyo akiba tayari ipo, unaona. “Yeye—Yeye—Yeye alijeruhija kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.” Unaona, yote yamekwisha. Nasi tunafurahi usiku wa leo kwa ajili ya imani yenu.

<sup>5</sup> Ninaamini Billy alikuwa akiniambia ndugu mmoja anatokea huko mbali sana Canada ama mahali fulani. Na je! hiyo ni kweli? Wewe ndiye huyo ndugu kutoka Canada? Na—na wewe unatoka wapi, ndugu? [Huyo ndugu anasema, “Kaskazini kidogo tu mwa Fort Wayne, katika Kendallville.”—Mh.] Kendallville, Indiana, kutoka Fort Wayne. Nilifunga ndoa huko Fort Wayne. Ninakumbuka vizuri. Nilifanya mikutano mingi kule, katika Maskani ya Redigar. Ninadhani mnajua iko wapi. Nami nakumbuka, nikiwa mvulana mdogo, nikiketi miguuni pa Paul Rader, kwenye Maskani ya Redigar, kama tu kijana mwanafunzi mhudumu. Yeye ni maarufu sana, Ndugu Paulo alikuwa maarufu, na vivyo hivyo Ndugu Redigar, mtu wa imani. Nafsi yao inastarehe usiku wa leo. Na sasa, kama nilivyokuwa mvulana mdogo, ninajaribu kuendeleza yale waliyoacha, yale Yesu aliyoliachia Kanisa Lake tangu zamani.

<sup>6</sup> Sasa, kwa imani yote niliyo nayo, ninakuja kuwaombea. Nami—mimi siji kwa kubahatisha tu. Hatutaki hata kidogo kuliendea jambo hilo namna hiyo. La, hilo si sawa. Tunakuja, tukiamini tutapokea yale tuliyoomba, unaona, tukijua ya kwamba Mungu ameliahidhi. Nasi tunakuja tukiwa na uhakika moyoni mwetu ya kwamba Kristo aliahidi, nanyi ndugu

mmejaribu kuweka imani yenu madhabahuni, mkafanya yote mwezayo, ninakuja kuweka yangu pamoja na yenu usiku wa leo. Mnaona?

<sup>7</sup> Na, sasa, tuna madhabahu kubwa inayoeua kukiangama mbingu, na juu ya madhabahu hiyo kuna Dhabihu yetu, Mwana wa Mungu. Unaona? Ni ile Dhabihu inayotoka damu. Mungu hawesi kuiangalia hiyo bila kuiheshimu, unaona, kwa maana Hilo ni Neno Lake, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye.”

<sup>8</sup> Nitamwomba Ndugu Neville, mzee wetu, kama atakuja mbele sasa pamoja nami tunapoenda. Ninataka kanisa lote... Vipi kama huyu alikuwa ni ndugu yako, mume wako, mwanaao, baba yako? Ni nanii wa mtu, ukumbuke. Hebu, kwa unyenyeketu wote tulio nao, tumkaribie Mungu sasa kwa ajili ya ndugu hawa. Na tuinamishe vichwa vyetu.

<sup>9</sup> Baba yetu wa Mbinguni mwenye rehema, tunaleta katika Uwepo Wako sasa, karibu na madhabahu ya neema, ingawa tunasimama karibu na benchi dogo la mbao, tuseme, hapa duniani, lakini imani yetu imeinuliwa hata kwenye yele madhabahu kuu inayowaka moto kule ng'ambo, ambako Yesu (ile Harufu ya kupendeza mbele za Mungu, ile Dhabihu ya Damu kutoka Kalvari.) Yeye aliyeshinda kila maradhi, kila ugonjwa, mauti, kuzimu, na kaburi, na kufufuka tena na kupaa Mbinguni, apate kuketi katika mkono wa kuume wa Ukuu Wake. Nasi, kwa imani, twaja, tukijiinua juu kule katika neema ya Mungu, kutamka juu ya madhabahu hii, kumwambia yule Muumba mkuu wa Mbingu na nchi, “Tupokee, Bwana, tunapokaribia katika Jina la Bwana Yesu.”

<sup>10</sup> Hawa hapa ndugu zetu, na mmoja wao anatoka mbele ya Fort Wayne, hapa nchini, na huyu mwingine ni kutoka Canada hapa chini, wamekuja kwa ajili ya wakati huu wa uchaji sana. Ni kati ya mauti na uzima, Bwana. Hawa hapa watu wawili, wangali wachanga, wangali wana huduma nydingi kwa ajili Yako, Bwana, askari wawili, Wakristo wanaokuamini Wewe. Naye adui ametupa mshale, na mshale huo wa sumu umepiga mahali fulani mwilini mwao, nao wamerudi, wamerudi nyuma kwenye hospitali ya neema ya Mungu, kwa ajili ya upatanisho, kwa ajili ya uponyaji, wapate kurudi vitani tena, wameinua ngao, wakienda vitani. Wao wamekuja kujiunga na jeshi la maombi pamoja nasi, Bwana. Nasi tunaenda kumkabili adui.

<sup>11</sup> Katika Jina la Yesu Kristo, waachilie. Tunakuapisha katika Jina la Yesu Kristo, waachilie.

<sup>12</sup> Wao ni mashujaa wa vita. Na, kama mtumishi Wako, ninaenda mbele sasa kuweka mikono yangu juu yao, kwa imani, nikiamini ya kwamba. “Ishara hizi zitafuatana ha hao waaminio,” alisema Bwana wetu, Kapteni wetu Mkuu wa vita, “wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

<sup>13</sup> Ninafanya jambo hili katika Jina la Yesu Kristo. Jalia nguvu za maradhi zinazoufunga mwili wa ndugu huyu, zimwachilie, katika Jina la Yesu Kristo. Nguvu za maradhi zinazoufunga mwili wa ndugu huyu, zimwachilie, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia...?...

<sup>14</sup> Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwazilishi wa Uzima wa milele, Mpaji wa kila kipawa chema, shusha baraka Zako juu ya hawa ambao tumewabariki. Na imeandikwa katika Maandiko, ya kwamba, "Ukuimbilia mlima huu, 'Ng'oka,' usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako." Ninaamini ya kwamba magonjwa yao yametoka mwilini mwao. Sasa imekuwa...?...Sasa na itendeke. Amina.

<sup>15</sup> Katika Jina la Bwana Yesu ninaamini wewe ni huru. Katika Jina la Yesu Kristo ninaamini wewe ni huru. Amina. Je! kanisa linaamini vivyo hivyo? Basi na itendeke.

<sup>16</sup> Sasa, kuna wengine hapa wangetaka tu kukumbukwa katika maombi, waweza kuinua mkono wako? Vema, hebu na tumkaribie sasa wakati mkiwekeana mikono huko mliko. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

<sup>17</sup> Mungu aliye mtakatifu sana, kwa imani tunamwona Yesu, tunaamini Yeye yupo amesimama. Yeye hulilinda Neno Lake. Naye alisema, "Mahali po pote wawili ama zaidi wakutanapo katika Jina Langu, Mimi niko katikati yao." Sasa, Baba wa Mbinguni, jalia nguvu za Mwenyezi Mungu ziguse watu hawa, Bwana, wakati wameshikana mikono, wamewekeana mikono. Agizo la mwisho uliloliambia kanisa, "Ishara hizi zitafuatana ha hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, wata-...watapata afya." Uliahidi jambo hilo, nasi tunaliamini. Kwa hiyo sasa limetimia, nasi tunakusifu kwa hilo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

<sup>18</sup> Na katika Jina la Yesu Kristo jalia nguvu za Mungu zitie mafuta leso hizo kwa ajili ya wagonjwa na wahitaji. Na zinapotumwa na kuwekwa juu ya wagonjwa, na iwe kwamba watapona. Tunasoma katika Biblia ya kwamba walichukua kutoka kwa Mtakatifu Paulo, leso, vitambaa; roho wachafu wakawatoka watu, na magonjwa yakaponywa. Na, Baba, tunajua ya kwamba sisi si Mtakatifu Paulo, bali tunajua ya kwamba Wewe ungali ni Yesu. Nasi tunaomba ya kwamba utatujalia haja hii kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

<sup>19</sup> Sijui kama ka—kanda zinanasa, ama hazinasi. Zinanasa? Kama hazinasi, ningewataka wazifungulie wakati huu. Ninaamini swichi imewashwa. Sasa, ninatumaini ya kwamba sitawachosha usiku wa leo. Ninaanza karibu nusu saa ama dakika thelathini na tano mapema. Na sasa, ni somo la shule ya Jumapili, nami nimedhani ya kwamba labda ingefaa kama

ningenasa jambo hili lililo moyoni mwangu. Nasi tuko karibu kuingia katika hatua m—mpya, maskani mpya, mpya kabisa.

<sup>20</sup> Na sasa ningetaka kusoma baadhi ya Maandiko. Kama ninyi watu mngetaka kusoma pamoja nami, ninataka kusoma kutoka I Samweli, mlango wa 8, na tunataka kuanzia kifungu cha 4 hadi cha 10; halafu basi, ili kuokoa wakati, cha 19 hadi 20. Nami nina kurasa nydingi za Maandiko na marejeo yaliyoandikwa hapa, hivi kwamba kama ninyi watu mna kalamu na penseli, ama cho chote kile, karatasi, kwamba mngetaka kurejea kwenye haya ama kuyaandika, mnawenza kuyachukua, ama, Bw. Maguire atakuwa nayo hiyo ka—ka—kanda.

<sup>21</sup> Nami ninataka kanda hii iwekwe wakfu kwa matumizi ya wahudumu, ndugu zangu, wahudumu ambao wamenielewa vibaya, hasa sana ndugu wa makanisa ya kimadhehebu. Na karibu wote ni wa madhehebu.

<sup>22</sup> Na somo langu usiku wa leo ni: *Kwa Nini Ninachukia Dini za Kimadhehebu*. Na nitasoma sasa kwa ajili ya kuweka msingi, ama somo la Maandiko, kulifanya la Kimaandiko hasa, ninataka kusoma kutoka I Samweli 8:4-10, halafu 19-20. Kwa wasikilizaji wangu walio hapa, ninatumaini ya kwamba mtakapoenda nyumbani kwamba mtaandika Maandiko haya na kuyasoma kwa makini. Na kwa ndugu watakaokuwa wakisikiliza kanda hii, ninatumaini ya kwamba ninyi pia hamtasimamisha tu kanda wakati jambo fulani limesemwa ambalo labda hamtakubaliana nalo, lakini kwamba mtamtafuta Mungu katika jambo hilo, mwone kama ni la Kimaandiko. Nafikiri ni jukumu letu na kwa Ujumbe wa siku hii.

<sup>23</sup> Ninaamini ya kwamba Makanisa yote yana Wakristo ndani yao, na bila shaka mimi sizungumzi dhidi ya Wakristo. Lakini sababu ya kufanya yale niliyofanya, na kusema yale miliyosema, ni kwa sababu ya uvuvio wa Roho Mtakatifu juu ya Neno.

<sup>24</sup> Sasa na tusome katika I Samweli, mlango wa 8, kuanzia kifungu cha 4, na kusoma cha 10, vyote pamoja, kwanza.

*Ndipo wazee wote wa Israeli wakakutana pamoja, wakamwendea Samweli huko Rama;*

*Wakamwambia, Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi... hawaendi katika njia zako; basi, tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote.*

*Lakini neno hilo likawa baya machoni pa Samweli, waliposema, Tupe mfalme atuamue. Naye Samweli akamwomba BWANA.*

*BWANA akamwambia Samweli, Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokukwambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao.*

*Kwa kadiri ya matendo yote waliyonitenda tokea siku ile nilipowatoa katika Misri hata leo, kwa kuniacha mimi, na kwa kutumikia miungu mingine, ndivyo wanavyokutenda wewe.*

*Basi sasa isikilize sauti yao; walakini, uwaonye sana, na kuwaonyesha desturi ya mfalme atakayewamiliki.*

*Naye Samweli akawaambia wale watu waliotaka mfalme maneno yote ya BWANA.*

<sup>25</sup> Sasa kifungu cha 19 na cha 20 kwa kumalizia.

*Walakini hao watu wakakataa kuisikiliza sauti ya Samweli; wakasema, Sivyo hivyo; lakini tunataka kuwa na mfalme juu yetu;*

*Ili sisi nasi tufanane na mataifa yote; tena ili mfalme wetu atuamue, tena atoke mbele yetu na kutupigia vita vyetu.*

<sup>26</sup> Bwana na aongeze baraka Zake katika kusomwa kwa Neno Lake. Sasa, kama darasa la shule ya Jumapili, ningetaka kusema ya kwamba tunataka kujitahidi kusikiliza Neno kwa—kwa makini sana tuwezavyo.

<sup>27</sup> Na tunajua ya kwamba—ya kwamba mara nyingi vitu vinasemwa, (na makanisa fulani), ambayo humkwanza mtu ambaye amefundishwa kinyume cha yale waliyo nayo... wanayosikia. Kwa mfano, mtu fulani aliniambia majuzi, ambaye ni rafiki yangu anayeketi hapa sasa, ye ye ali sema, “Wakati uliposema, Ndugu Branham, kadiri nilivyokuwa na imani kubwa kwako, na kuamini, wakati uliposema hapakuwepo na ‘jehanamu ya Milele,’” kasema, “karibu nianguke kutoka kwenye kiti changu. Ndipo nikasema, ‘Hakika mtu huyu amekosea.’” Halafu akasema, “Ulitufanya tusimame kwa muda mrefu sana. Kisha ukasema, ‘Kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo hutokana na Mungu.’” Na huo ndio sisi sote tunaotafuta, unaona.

<sup>28</sup> Wala hakuna Maandiko yanayosema kuna jehanamu ya Milele. Maana, Milele kamwe haikuanza, wala haitaisha kamwe. Kwa hiyo Biblia ilisema “jehanamu iliumbiwa Ibilisi na malaika zake,” kwa hiyo si ya Milele. Kulikuwa na wakati ambapo haikuwapo, na kutakuwa na wakati ambapo haitakuwapo, tena. Lakini wao wanawenza kupewa adhabu huko, kwa moto na kiberiti, na mashimo ya moto, kwa kipindi kisichoweza kupimika, lakini hatimaye itaisha kwa sababu jehanamu si ya Milele. Na kama kulikuwako na kuzimu ya Milele, ingalikubidi uwе na Uzima wa Milele upate kuishi katika jehanamu ya Milele. Na kama ingalikuwa ya Milele, basi ilikuwa ipo daima, nawe daima ulikuwa uko jehanamu na daima utakuwa jehanamu. Unaona, kwa hiyo hakuna kitu kama hicho.

<sup>29</sup> Kwa hiyo, unaona, *Milele* ni “pasipo na mwanzo wala mwisho.” Na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na hiyo imo katika Mungu, inatokana na neno la Kiyunani *Zoe*, ambalo maana yake ni “Uzima wa Mungu Mwenyewe.” Na tunapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, tunakuwa wa Milele pamoja na Mungu, kwa sababu tuna sehemu ya Uzima Wake, ambao unatufanya wana na binti za Mungu, ndipo tuna Uzima wa Milele. Na Uzima ule ulio ndani yetu, Mungu ataufufua mwili pamoja na Uzima huo katika siku ya mwisho, lakini ni Roho wa Mungu aliye ndani yetu anayefufuka, kwa maana ni Roho wa Kristo aliye kuwa katika Kristo, ambaye huihuisha miili yetu na kutufufua pia, pamoja Naye, kuketi katika—katika—katika Utukufu na kutawala pamoja Naye.

<sup>30</sup> Sasa tuliedee somo, sasa, ambalo nimelipitia miaka hii, na ambalo maskani hii inatetea. Ingawaje, nilifanywa mhudumu katika kanisa la Kimishenari la Batisti, na Daktari Roy E. Davis, yapata miaka thelathini na mitatu iliyopita, hapa katika Jeffersonville. Sasa mimi, tangu wakati huo, nilikuwa katika madhehebu kwa muda mfupi tu, miezi michache, mpaka jambo fulani lilipotukia kanisani lisilokuwa la Kimaandiko, nami nikamwambia ya kwamba nisingekubaliana na hilo. Na kwa hiyo mimi, bila shaka, niliambiwa “nifanye hivyo la sivyo,” nami nikalikataa. Kwa hiyo hilo likuwa ni jambo moja ambalo ninaamini, ya kwamba hili ni Neno la Mungu. Nami nikamwambia huyo mtu ambaye alikuwa ndiye mwalimu ho—hodari, “Kama utanionyesha jambo hilo katika Neno la Mungu!”

“Lakini likuwa,” yeche akasema, “hilo ni fundisho letu.”

Nikasema, “Lakini ninataka nilione katika Neno, unaona, Neno la Mungu.”

<sup>31</sup> Na si kwamba ati mimi si mfuasi wa madhehebu fulani ndiyo sababu nimekuwa nikiyapinga madhehebu, kwa sababu ninashukuru kwa ajili ya ndugu zangu, ambao ninawazungumzia leo, ambao hunialika, nadhani, karibu kila madhehebu, hasa sana katika makundi ya Injili Yote, na hata katika mengi ya makanisa hayo mengine. Nimeshaombwa kuhudhuria ushirika wao na kujiunga nao, lakini nimeishi huru. Kwa sababu, ushawishi nilio nao, sitaki kuweka juu ya kundi moja la watu. Ninataka kuweka yale ambayo Mungu amenipa, maombi kwa ajili ya wagonjwa, kuwafaidi watoto wote wa Mungu katika kila madhehebu. Yeche kamwe hajaniuliza nisiombe, ama kwa mtu fulani huyu ati kwa sababu yeche ni mfuasi wa *Kadha-na-kadha*, Mungu huhukumu moyo wa mwanadamu.

<sup>32</sup> Na sasa, kwanza kabisa, sababu ya mimi kwamba sikuwa mfuasi wake na nimeyapinga, ni, kwanza, ni kwa sababu siamini ya kwamba kuunda madhehebu ya Kikristo ni jambo la Kimaandiko. Ninaamini si jambo la kimaandiko. Na hiyo

ndiyo sababu nitajaribu, usiku wa leo, kujitahidi sana kwa neema ya Mungu, kuwathibitishieni ya kwamba ni jambo lisilo la kimaandiko, wala si halali kuunda madhehebu yo yote.

<sup>33</sup> Bila kukawia, kwanza kabisa, tunaiita “dini,” neno *dini* linamaanisha “kifuniko,” linamaanisha kufunika kitu fulani. Sasa, Adamu alikuwa na dini, bali bila shaka aliifanya ye ye mwenyewe, kutokana na majani ya mtini, wala haikufaa kitu. Alijibunia nadharia yake mwenyewe na kujaribu kupata mlango wa kutokea, ili apate wokovu katika kitu alichokuwa amefanya mwenyewe, na Mungu akakikataa, tangu Adamu hadi utaratibu wa madhehebu ya mwisho. Hajapata kukikubali, na kwa neema ya Mungu tutathibitisha jambo hilo leo kupitia kwenye Biblia. Dini ilikuwa ni kifuniko. Adamu alijitengenezea kifuniko kutokana na majani ya mtini, akajitengenezea, ye ye mwenyewe, kujaribu kufanya jambo fulani ye ye mwenyewe.

<sup>34</sup> Lakini Mungu alihitaji mauti, upatanisho. Sasa, kuna tofauti kubwa sana kati ya dini na wokovu, unaona, wokovu. Dini ni kifuniko. Unaona? Wokovu ni Kuzaliwa, karama ya Mungu. Wokovu ni Kuzaliwa, karama ya Mungu, wala hauwezi kupatwa na mtu ye yote wala kundi lo lote la mwanadamu. Mungu humletea mtu binafsi karama hii. Na karama hizi za Uzima wa Milele zilikusudiwa na Mungu kwa ajili ya kila mtu binafsi kabla hata hatujakuwa na ulimwengu, kulingana na Maandiko. Biblia ilisema, katika Ufunuo, ya kwamba mpinga-Kristo aliyekuwa aje juu ya nchi, angewadanganya wote walioishi juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Unaona? Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, aliona ni nani angekuja na ni nani asingekeuja, Kristo alishuka kufanya njia kwa ajili ya wale ambao wangekuja. Unaona, kuwajua hao wengine.

<sup>35</sup> Kama Yeye ni Mungu, kweli, hana budi awe hana kikomo. Na kama hana kikomo, Yeye hawezi kuwa hana kikomo bila kuwa mwenye nguvu zote. Hawezi kuwa mwenye nguvu zote bila kuwa yuko kila mahali. Hawezi kuwa anayeenea kila mahali bila kuwa mwenye kujua yote. Kwa hiyo, unaona, yote hayo yanamfanya Yeye kuwa Mungu.

<sup>36</sup> Kwa hiyo, Yeye alijua mwisho tangu mwanzo. Yeye alijua ni nani atakuja na ni nani hatakuja, na alijua kutakuwako na wengi watakaokuja, kwa hiyo akamtuma Kristo kufanya upatanisho kwa ajili ya hao ambao wangekuja. Sasa, hakuna jambo tunaloweza kufanya lililo na uhusiano wote na jambo hilo. Yesu alisema, “Wote alionipa Baba,” alionipa wakati uliopita, “watakuja Kwangu. Wala hakuna mtu anayeweza kuja asipovutwa na Baba.” Unaona? Sasa, unaona, yote yako katika kujua Kwake Mungu.

<sup>37</sup> Unasema, “Ndugu Branham, je! mimi nimo ndani?” Sijui. Ninatumaini ya kwamba nimo. Tunatimiza wokovu

wetu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Sasa, Kanisa limechaguliwa kukutana na Mungu bila waa wala kunyanzi. Sasa, kama tuko katika Kanisa Hilo, tumechanguliwa tangu awali kwenye Kanisa hilo. Sasa jichunguzeni kwa Neno, Ndipo mnapoweza kuangalia tuko umbali gani.

<sup>38</sup> Sasa, basi, Ukristo wa kimadhehebu hauwezi kuleta matumaini hayo. La. Baadhi yao walisema, “Unakuja na kukiri ya kwamba Yesu ndiye Kristo na ubatizwe kanisani.” Ibilisi hufanya jambo lile lile. Anaamini, ye ye mwenyewe, ya kwamba Yesu ndiye Kristo, na anatetemeka. Unaona, hiyo ni kweli

<sup>39</sup> Mungu hakuamuru kamwe, mahali po pote katika Maandiko, panaporuhusu kuwepo kwa madhehebu. Hakuna nafasi katika Biblia kwa jambo hilo. Adamu alianza moja nayo ikashindwa.

<sup>40</sup> Halafu Nimrodi akajaribu kuunda madhehebu. Kama wewe ni mwanahistoria, na unajua historia ya Babeli, soma *Babeli Mbili*, kilichoandikwa na Hislop, utapata nuru nyingi sana. Huyo, Nimrodi, huyu mtu wa dhambi, aliitwaa Babeli pamoja na makanisa yake madogo mashirika, ama sehemu zilizoizunguka, jambo ambalo lilikuwa ni mfano wa—wa ukengeufu huu wa Ukristo wa mwisho, na akafanya mahali pamoja pakubwa mno na hao wengine wote wakacheza... wakapalipa kodi. Na mle ndani akajenga mnara na kujaribu kuwakusanya watu pamoja, lakini halikufanikiwa. Halikufanikiwa. Hilo lilishindwa.

<sup>41</sup> Kora, katika Hesabu 16:1, kama mngetaka kusoma, Kora alijaribu jambo lile lile. Aliwakusanya Walawi wote, na akawakusanya... baadhi ya watu mashuhuri, watu wa tabaka la juu, watu wakuu, watu watakatifu, naye pamoja na Dathani wakakutana na kusema, “Si haki, mtu mmoja kujaribu kututawala sisi sote.” Na kwa hiyo wakajaribu kuanzisha kuunda madhehebu kwa pamoja, ndipo wakamwendea Musa na Haruni, ambao Mungu alikuwa amewachagua kwa ajili ya hiyo kazi, na kuwaambia ya kwamba wamejiinua sana, ya kwamba kusanyiko lote lilikuwa takatifu, nao walikuwa na haki ya kuninii... “Kwa wingi wa mashauri huja wokovu,” bila shaka, wao wanasema hivyo. Huo hautumiki kwa Ukristo. Huo ni katika vita. Angalia, tofauti kubwa sana.

<sup>42</sup> Unaweza kuchukua Maandiko, na kusema, “Yuda alitoka akaenda akajinyonga” na “wewe nenda ukafanye vivyo hivyo,” ukitaka, lakini hilo halilifanyi kuwa sawa.

<sup>43</sup> Mungu alikuwa amemchagua Musa na Mungu alikuwa amemchagua Haruni, na ulikuwa ni ujumbe wa siku hiyo. Na haidhuru jinsi upando huo mwininge ulivyoonekana kuwa mzuri, ulikuwa ni kinyume cha mawazo ya Mungu. Na hatuna budi kuacha mawazo ya Mungu yawe ni mawazo yetu. “Iwени na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo ndani ya Kristo.” Na Biblia hii inafunua nia ya Kristo. Na Kitabu chote kizima

cha Ufunuo, kinachoitwa Ufunuo, ni Ufunuo wa Yesu Kristo. Nasi tunaweza kuona jinsi anavyohukumu kitu hicho, jinsi anavyokichukua upande mmoja, na tutalifikia jambo hilo baada ya kitambo kidogo. Vema.

<sup>44</sup> Kora, ninaamini ye ye aliкуwa mwaminifu katika tendo lake. Ninaamini mtu huyo haku—hakukusudia kufanya mabaya. Ninaamini ni kutojua kwa mtu huyo ambako hakukuona mkono wa Mungu ukitenda kazi na kujua Maandiko, na hiyo ndiyo sababu ye ye alilihoji.

<sup>45</sup> Na hiyo ni kama asilimia tisini ya shida za siku hizi, ya kwamba sisi hujaribu kuingiza katika mpango wa Mungu, mawazo yetu. Wala hatupaswi kuwazia, hata kidogo. Yeye ndiye anayetuwaszia. Tunapaswa kuyatiisha mawazo yetu kwa mapenzi Ÿake. Mnafahamu jambo hilo sasa?

<sup>46</sup> Kora, akiwa na mawazo mazuri, alienda kila mahali na fundisho la uongo, akiwaambia hawa ndugu, na kuwaonyesha kwa hoja, ya kwamba Mungu hakuwa amembariki Musa peke yake tu, yule nabii, yule mjuimbe, na aliкуwa tu amembariki, lakini, “Kusanyiko lote lilikuwa takatifu,” akasema, “na sasa kusanyiko lote lina haki ya kufanya jambo *hili*, na kusanyiko lote lina haki ya kufanya *vile*.” Na kwa hiyo wakatwaa watu wazuri, Walawi. Sasa, hao walichaguliwa na Mungu, ambao wangeitwa leo, “wahudumu,” Walawi walikuwa wahudumu wa hekalu. Je! Musa hakuwaitia jambo hili? Na, hapa, ye ye hakuingilia jambo hilo bila... bila uchaji. Aliwaambia wachukue vyetezo, na kuweka moto mtakatifu ndani yake, na kuweka uvumba juu yake, na kutikisa uvumba huu mtakatifu, ambayo ilikuwa ni amri ya Mungu. Nao wakaja kuunda kundi la watu lilitawale kanisa, ambapo Mungu aliкуwa ameamrisha mtu mmoja kultawala.

<sup>47</sup> Na, walipofanya jambo hilo, Musa alianguka kifulifuli kwa kuwa alijua ya kwamba Mungu aliкуwa amemwagiza kufanya kazi hiyo. Ndipo Mungu akasema, “Waambie walete vyetezo hivyo hapa mbele ya ile maskani.” Na kwa hiyo walipoanza kufukiza kwa vyetezo vyao vilivyojaa moto, na uvumba unaendelea, Mungu akamwambia Musa na Haruni, “Jitengeni nao! Tokeni kati yao!” Kwa kuwa, baadaye aliwaita “wenye dhambi, wasioamini.”

<sup>48</sup> Na dhambi ni kutokuamini katika Neno la Mungu. Unaiba kwa sababu huamini. Unasema uongo kwa sababu huamini. Unafanya uzinzi kwa maana huamini. Kama ungekuwa ni mwamini, hungefanya mambo hayo. Kuna mavazi mawili tu, hayo ni aidha imani ama kutokuamini, unatawaliwa na moja ama lingine.

<sup>49</sup> Sasa, Mungu, hapo mwanzo, aliкуwa Neno, Naye alifanyika mwili akakaa kwetu. Yeye aliкуwa Neno, Yeye ni Neno! Na wakati Mungu anapokaa ndani yako, Ni Neno la Mungu

likiishi ndani yako, ambapo unaweza kuitikia kila kitu Yeye anachosema kwa "Amina." Huyo ni Mungu akiishi ndani yako.

<sup>50</sup> Sasa kama ukiangalia, hawa watu wasio na hatia wakiwa na vyetezo mkononi mwao, moto mtakatifu mkononi mwao, Mungu aliifungua ardhi ikawameza, na kuwatenga na Musa kwa sababu Musa alijitenga nao. Ndipo Musa akalionya kusanyiko, "Msijipumbaze na kundi la namna hiyo. Likimbieni!" Sasa, mnajua Maandiko, someni mlango wa 16, 17, 18, hata, mlango, na mtalipata. "Jitengeni na hawa wenye dhambi, wenye dhambi wasioamini. Tokeni kati yao, kwa kuwa wanaelekeea kwenye maangamizi, na kila walicho nacho." Na wakati wao...ardhi ilipasuka na kuanguka pamoja na watu hawa waliokuwa wameshika huu moto mtakatifu. Watu wasio na hatia waliodanganywa na mwanadamu.

<sup>51</sup> Ndivyo ilivyo leo! Kuna watu wengi wasio na hatia wanaoanguka katika mtego wa mapokeo, wameshika Neno Takatifu mikononi mwao, na wakidhaniwa wanalihubiri. Nimeona sura ya mhudumu ikibadilika sasa hivi, mhudumu wa Kimethodisti, alikuwa mhudumu wa Kimethodisti mpaka Jumapili iliyopita usiku. Na wakati alipoangalia, nadhani inamaanisha mengi sana kwako, ndugu, kutoka nje.

<sup>52</sup> Sasa, unaona, wakashika vyetezo, moto ukioka harufu nzuri mbele za Mungu, na mikono hiyo ikishika hivyo, hata hivyo wakaangamia wakiwa na vyetezo hivyo mikononi mwao, kwa sababu walikuwa wakijaribu kufanya jambo fulani kwa uaminifu, hata hivyo, ni kinyume cha Neno la Mungu, wakijaribu kuunda madhehebu. Kasema, "Unajiinua sana. Wewe ni nani kusema una Neno lote la Mungu?"

<sup>53</sup> Walishindwa kuona ya kwamba Musa alikuwa ni m—mjjumbe wa saa hiyo. Unaona, alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Hapakuwapo na mtu duniani kama yeye. Alikuwa na Ujumbe, na watu walikosa kuona jambo Hilo. Naye Musa alikuwa na BWANA ASEMA HIVI hasa. Hakika. Vema.

<sup>54</sup> Sasa tunaona jambo lile lile leo, watu wazuri, watu wakuu, watu wa thamani wakijaribu kuhubiri Neno la Mungu (mkononi mwao) kupitia mapokeo yaliyotungwa na mwanadamu. Wakikata *hana*, na kukata *hana* chini, na kulifanya *hivi*, na "njoo ujiunge na kanisa na ubadilishe kanisa lako," nao wanakufa kiroho wakiwa wameshika Neno hilo mkononi mwao! Unaona?

<sup>55</sup> Wao hawakuweza kumwamini mjumbe wa Mungu au Ujumbe Wake wa siku hiyo. Hawakuweza kufahamu ni kwa nini Mungu mkuu asingetenda kazi na kundi kubwa la watu, na aiweke tu juu ya mtu mmoja.

<sup>56</sup> Ni wangapi wao nimezungumza nao leo, "Tutafanya nini, Ndugu Branham? Tunajua ya kwamba unasema kweli, lakini tufanye nini? Madhehebu yatatufukuza, hatutakuwa na mahali

pengine pa kwenda.” Ninawasikitikia; lakini kuna Mahali fulani. Unasema, “Vema, tungekufa njaa.”

<sup>57</sup> Daudi alisema, “Nalikuwa kijana wakati mmoja, nami sasa ni mzee, wala sijamwona mwenye haki ameachwa, wala mzao wake akiomba chakula.”

<sup>58</sup> Vivyo hivyo kwenye msingi huo huo ndivyo walivyomkataa Yesu. Walikuwa wamejifunga sana katika madhehebu yao, na makuhani watakatifu na majengo matakatifu, na makanisa matakatifu na mahekalu matakatifu, walishindwa kumwona Mungu katika hekalu Lake la kibinadamu. “Wewe, ukiwa mwanadamu, unajifanya mwenyewe Mungu.” Unaona, walikuwa wamejifunga sana kwake! Watu hawa walikuwa wamejifunga sana hivi kwamba Dathani na hao wengine walikuwa sahihi. Nimrodi alikuwa amejifunga sana hivi kwamba angefanikiwa katika kitu fulani ambacho kingewachukua watu juu ya hasira ya Mungu. Adamu alikuwa na hakika ya kwamba kama angefunika uchi wake Mungu hangeweza kuuona. Huwezi kuufunika, inabidi Mungu aufunike. Unaona? Unaona? Utaratibu wa Mungu ndio unaoufunika, si wako. Imekuwa hivyo sikuzote, wao wanashindwa kumwona Yesu katika hekalu Lake, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

<sup>59</sup> Siku hizi linanifanya nijisikie vibaya wakati nikiona ya kwamba Maneno ya Biblia yamekatwa-katwa sana na mapokeo. Na watu wenyewe miyo miaminifu wanaosimama pale na kulisikia Neno hilo, nao wanajua kwamba ni Kweli, bali hawathubutu kufanya lo lote, kwa sababu mapokeo yao yanawafundisha vinginevyo. Osheni vyungu na midumu, basi, enyi ndugu, endeleeni. Lakini kwetu sisi, na kwangu mimi na nyumba yangu, tunamchukua Kristo, Neno. Unaona?

<sup>60</sup> Hebu na tuchukue Yohana 3 kwa muda kidogo tu, Nikodemo, mwalimu na mtawala wa madhehebu makubwa yaliyoitwa Baraza la Wazee. Walikuwa wamekusanyika pamoja, nao wakafanya mapokeo yao. Mo—moja ya Mafarisayo na moja ya Masadukayo, nao walikuwa na madhehebu yao wakati huo, tofauti zao, na kwa hiyo wao... Mtu huyu alikuwa mwalimu, mtawala wa Baraza hili kuu la Wazee, mtu hodari sana katika kufundisha. Yeye aliyafahamu Maandiko, ndivyo aliyodhani. Aliyajua kwa mapokeo yao. Je! Yesu hakusema, “Ninyi, kwa mapokeo yenu, mmezitangua amri za Mungu”?

<sup>61</sup> Unaona, kwa sababu ya mapokeo yao! Ni kitu gani hicho? Kuweka fasiri zao wenyewe juu ya Neno, badala ya kuliacha peke Yake, yale linayosema. Wao wanasema halimaanishi Hivi. Je! umegundua, hiyo ndiyo sauti ile ile ambayo Ibilisi alitumia kwa Hawa, kuanzisha madhehebu ya kwanza, unaona. “Hakika lingepaswa kuwa *hivi*. Mungu asingefanya jambo hilo, unajua.” Unaona, ni kitu kile kile. Ni kitu kile kile.

<sup>62</sup> Sasa tunaona mtawala huyu alikuja kwa Yesu. Jambo la kwanza, sasa, alikuja kutafuta Uzima wa Milele, alikuja kutafuta wokovu. Hata hivyo, mtu wa wadhifa wake, mwalimu wa Israeli, lakini mwalimu wa Israeli alimjia Mtu ambaye hatuna taarifa kwamba alipata kwenda shuleni hata siku moja. Mwanamume, kuhani mzee, mwenye hekima, akamjia Jamaa mmoja mdogo. Wao walikuwa ni makabaila, tajiri akamjia Mwombaji asiyekuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake, kumwuliza amwelekeze kwenye njia ya wokovu na Uzima. Kwanza, hao wanachama wa Baraza la Wazee, Nikodemo alikiri, walikuwa wameona kitu fulani katika Yesu ambacho mtu mwagine wa madhehebu yao hakuwa nacho. Waliona kwamba kulikuwako na jambo fulani ndani Yake, kwa sababu yeye alisema, “Rabi, tunajua Wewe.” “Sisi,” naam, wao hawangekiri jambo hilo, kwa sababu wangetupwa nje. Unaona? “Tunajua Wewe ni Mwalimu aliyetoka kwa Mungu, kwa kuwa hakuna mtu angeweza kufanya mambo haya ufanyayo Wewe, isipokuwa Mungu awe pamoja naye. Tunajua jambo hilo!” Loo, jamani! Madhehebu!

<sup>63</sup> Sasa, tunaona ya kwamba Yesu alikuwa ni dhihirisho la Mungu. Sasa, “Hakuna mtu awezaye kufanya mambo haya isipokuwa Mungu awe pamoja naye.” Wao walijua kulikuwa na kitu tofauti katika Mtu huyo. Yeye alikuwa Nuru ya wakati huo. Alikuwa ni Shahidi wa Mungu.

<sup>64</sup> Vivyo hivyo Kora aliona jambo lilo hilo katika Musa. Hawakuwa na mtu siku hiyo kama Musa. Yeye alikuwa shahidi Mtakatifu wa Mungu, wa siku hiyo, kwa nguvu za Mungu. Kora na kundi lake waliona jambo hilo kwa Musa. Walifahamu ya kwamba haingeweza kuwa ni Musa; Musa asingeweza kuifungua Bahari ya Shamu, Musa asingeweza kutuma mapigo duniani. Ilikuwa ni Mungu ndani ya Musa, na, kwa sababu kwamba Mungu aliyejiwakilisha Mwenyewe katika shahidi ama nuru ya wakati huo, wao walikosa kuona jambo Hilo. Kora alitaka kuwa na kundi zima la watu, aingize kitu cho chote.

<sup>65</sup> Hiyo ndiyo kazi ya madhehebu, kuleta akina yahe wawezao kupata, na kuita hilo ni “Ukristo.” Wanapeleka mvulana shuleni asiyejua zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhotentoti angejua kuhusu shujaa wa Kimisri, wanampeleka huko na kumpa elimu na kumfundisha saikolojia, na kumpa Ph.D., na digrii ya juu kabisa ama digrii ya sanaa, ama kitu kama hicho. Na kumpeleka akahubiri Injili, mtu ambaye hata hajapata kuokolewa, ambaye atakana kazaliwa kibikira na ufufuo, anakana kuponya Kiungu, anakana Nguvu za Mungu, anakana kanuni zenyewe hasa ambazo Kristo alifia, anakana Marko 16 kwamba imevuviwa, anakana “ishara hizi zitafuatana na hao waaminio” wakati Yesu ndiye aliesema Maneno hayo Mwenyewe, anakana Matendo 2:38, anakana Maandiko mengine yo yote hayo ambayo yamevuvuviwa. Na kujaribu kuchukua

mapokeo ya mwanadamu wasiojua kitu juu yake, na kusisitiza jambo hilo. Na unapowaambia Kweli na kuwaonyesha Kweli, wanaona aibu kufanya lo lote, kwa sababu ya madhehebu yao.

<sup>66</sup> Kora alifanya jambo lile lile, walimwona Mungu katika Musa, aliona kwamba lilikuwa ni Mjumbe wa Mungu akitenda kazi kuititia kwake. Naye Nikodemo alimwona Mungu katika Kristo, “Hakuna mtu awezaye kufanya mambo haya isipokuwa Mungu yu pamoja naye.” Nikodemo alikuwa tayari katika madhehebu, akijaribu kutoka. Kora alikuwa nje, akijaribu kuunda moja apate kuingia ndani yake. Tofauti yake ilikuwa ni hiyo. Nikodemo alikuwa akijaribu kupata wokovu, apate kutoka katika kitu hicho; alikuwa ndani yake tangu alipokuwa mvulana, alikuwa amechoshwa nacho. Alitaka kuokolewa. Lakini Kora alikuwa akijaribu kuijandalia ma—mahali ambapo angeweza kuwa mtu mwénye cheo kikubwa.

<sup>67</sup> Hivyo ndivyo ilivyo kwa watu leo. Hiyo ndiyo shida ya Ukristo, tuna uigizaji mwinci wa uongo. Na watu wetu wa Kipentekoste, samahani kwa msemo huu, ni wabaya sana kwake, kujilinganisha kimwili! Hebu Mungu amwinue mtu fulani na kumpa kitu fulani, na kila mtu nchini atajaribu kumwiga mtu huyo. Je! hamtambui ya kwamba mnaua timu yenu wenyewe? Mnapocheza soka... “Na neema,” kama vile ambavyo Paulo alilisema, “na tupige mbio hizi kwa saburi.” Mtu aliye na Mpira huo, usiupokonye kutoka mikononi mwake, jaribu kumlinda. Lakini badala ya kufanya hivyo, kwa sababu yeye si wa madhehebu yenu, unajaribu kumpokonya. Mtu ambaye ni goigoi sana, hangeweza, angejikwaa kwenye maua yaliyo kwenye zulia, na halafu anajaribu kukupokonya Huo. Hiyo ni kweli. Sasa, tukineni kiroho, ninamaanisha. Samahani, mimi... Vema, yeye atajikwaa juu ya kitu kidogo kama Matendo 2:38, bila shaka ataanguka. Kama kamwe akijikwaa kwenye Marko 16, atafauluje? Unaona? Masomo rahisi sana ya Kristo. Na jambo lile lile lililozungumziwa kwenye Baraza la Nikea, wangali wanajikwaa juu yake baada ya miaka hii yote.

<sup>68</sup> Kujaribu, Kora alikuwa akijaribu kuunda madhehebu, kuingia ndani yake. Naye Nikodemo alikuwa ndani yake, akijaribu kutoka humo. Nikodemo alikubalika, kisha akatoka. Kora aliangamia mle, katika jitihada zake, aliangamia katika jitihada zake mwényewe. Loo, jamani!

<sup>69</sup> Madhehebu aliyokuwemo Nikodemo, ilijua ya kwamba Kristo alikuwa ametumwa na Mungu, ilisema hivyo. Nikodemo, katika mlango wa tatu hapa, anakiri jambo hilo, “Rabbi, tunajua ya kwamba Wewe u Mwalimu aliyetumwa na Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kuifanya miujiza hii uifanyayo Wewe isipokuwa Mungu yu pamoja naye” Na kundi lilo hilo, kwa sababu ya madhehebu yao, llimwita “Beelzebuli,” kwa sababu ya nguvu Zake za kutoa pepo, na wakasema, “Yeye

anawadanganya watu wetu kwa Fundisho Lake.” Ni jambo lile lile leo. Ati kudanganya nini?

<sup>70</sup> Yesu alisema, “Mimi hufanya yale tu yampendezayo Baba, Mimi hutii tu Maneno ya Mungu,” kwa maana Yeye alikuwa ni Neno. Hakuweza kufanya jambo lingine isipokuwa Neno.

<sup>71</sup> Lakini, kwa sababu ya madhehebu yao, kwa sababu ya njia zao, walimfunga mtu huyo. Katika mioyo yao walijua jambo hilo, lakini madhehebu yao yasingewaruhusu kulitii. Halafu, ili kufanya njia ya kutokea, kuwazuia watu wasiyaache madhehebu yao (“watu wote wanamfuata Yeye”), ili kuwazuia watu wasiondoke kwenye madhehebu na kuifuata Kweli ya Mungu (ambapo Yeye alikuwa Kweli “Mimi ni Kweli, Nuru”) ili kuwazuia wasiifuate Hiyo, wakasema ya kwamba alikuwa anawadanganya watu. Wazia jambo hilo! Mtu, ambaye ndani ya moyo Wake alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, ya kwamba Mungu alikuwa ndani Yake (“hakuna mtu awezaye kusema mambo haya, ama kufanya mambo haya, isipokuwa Mungu yu pamoja naye”), akijua jambo hilo na kusema hivyo na kukiria jambo hilo, halafu wanageuka na kumwita “Beelzebuli, na mwenye kuwadanganya watu,” watu wao, “kwa Mafundisho Yake.” Loo, jamani!

<sup>72</sup> Nikodemo alijua Yeye alikuwa ni Nabii. Sasa, huyo alikuwa ni mtu mmoja katika madhehebu ambaye alimpenda Mungu vya kutosha na kumcha Mungu vya kutosha, na akatambua kwa Agano la Kale ya kwamba Mtu huyu alikuwa na zile sifa na amehakikishwa na kuthibitishwa, kwamba ni Nabii aliyetumwa na Mungu. Mtu huyo, nitamheshimu, hata ingawa yeye alikuja usiku, alivasili. Yeye ni bora zaidi ya baadhi ya waalimu wetu siku hizi, wao hawatakuja kamwe. Hatimaye Nikodemo aliwasili. Kwa hiyo, usimlaumu, kama wewe hujawasili bado. Nikodemo alijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Nabii, kwa hiyo alimcha Mungu. Yeye hangeruhusu Mtu huyo amwache, Nuru ya siku hiyo. Haidhuru ilikuwa ni kinyume namna gani, jinsi gani madhehebu yake yalisema yalikuwa vinginevyo, yeye alimwona Mungu akimthibitisha Mtu huyo naye alijua Yeye alikuwa ni Nabii. Na kama alikuwa ni Nabii, Neno la Bwana humjia nabii, Naye alijua alichokuwa akizungumzia. Unaona? Kwa hiyo akamwendea Yesu, alitaka kujua jinsi ya kupata wokovu. Mtu huyu alikuwa ni Nabii, Neno la Mungu lilikuwa pamoja Naye, Naye angejua njia ya wokovu.

<sup>73</sup> Lakini kile Nikodemo alipaswa kujua ni kile watu wengi siku hizi, wa madhehebu ya siku hizi, wanachopaswa kujua. Kile Nikodemo alichopaswa kujua, ni kile watu wa siku hizi walipaswa kujua, wa haya madhehebu. Yeye alikuwa ni zaidi ya Nabii. Yeye alimjia apate kujua, kumwambia amwambie ni njia gani ya Uzima, na Yesu Mwenyewe alikuwa ndiye Uzima. Yeye aliye na Mwana ana Uzima. Kwa hiyo yeye hakuninii, haikumpasa kuja kujifunza fundisho fulani, hana budi kuja

amkubali yule Mtu. Hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo! Lile Jiwe Kuu la Pembeni limekataliwa tena. Jiwe Kuu la kuwekwa Pembeni ni lipi? Ni Neno, bila shaka. Kristo, Yeye ni Neno.

<sup>74</sup> Ilimbidi ajifunze jambo fulani. Yeye aliwazia, “Vema, sasa, Mtu huyu ni Nabii, Yeye ni Nabii tu.”

<sup>75</sup> Kwa hiyo, hivi uligundua, Yesu hakulijibu swali lake, alimkemea tu kwa ajili ya upofu wake. Zaidi ya Nabii, Yeye alikuwa ni Neno na Mwanga unaomulika wa Neno! Yeye alikuwa ni Mungu akiangaza kupitia chombo fulani, ikithibitisha ya kwamba iliwa ni Mungu katika Mtu huyo. Yeye alikuwa ni Neno. Yohana wa Kwanza, mlanga wa 1... Yohana Mt., mlanga wa 1, hasa, inasema, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu” Na hapa palikuwapo na Neno la Mungu likiangaza kupitia kwa maskini mwili huu mnyonge wa Mtu, nalo likayapofusha madhehebu. Lakini Yeye alikuja kuwachukua watu binafsi. Zaidi ya Nabii, Yeye alikuwa ni Neno! Yeye ni Uzima. Si... Haikumbidi kukufundisha Uzima fulani ujao, Yeye Mwenyewe alikuwa ndiye huo Uzima! Alikuwa Uzima. Alikuwa Nuru. Alikuwa Uzima. Alikuwa Uzima wa Milele, ulikuwa ndani Yake, Naye pekee Ndiye Mpaji wa Uzima wa Milele. “Yeye aliye na Mwana yuna Uzima.” Kwa hiyo huna budi... huwezi kuwa tu na mafundisho ya Neno juu Yake, inakubidi kumpata Yeye.

<sup>76</sup> Unasema, “Loo, watu wanaketi na kujifunza hiyo Biblia na maneno yote ya Kiyunani, na maana yake, na vituo, na kadhalika.” Na hata hawamjui Mungu hata kidogo! Unaona? La! Yeye aliye—yeye aliye na m—m—mfano, yeye aliye na ramani? Ni yeye aliye na Mwana, aliye na Yeye, yule Mtu. Yeye Ndiye aliye na Uzima.

<sup>77</sup> Nikodemo alijua ya kwamba Yeye alijua habari za Uzima, lakini hakujuua kamwe ya kwamba Yeye alikuwa ni Uzima wa Milele. Huyo ndiye Mtu aliyekuwa anazungumza naye, yule Mjumbe, Nuru ya siku hiyo, Nuru ya ulimwengu. “Nuru hung’aa gizani, wala giza halikuiweza. Alitumwa kwa walio Wake wala walio Wake hawakumpokea.” Kwa nini? Kwa nini? Kwa sababu walikuwa wamezama kweli kweli katika madhehebu, wamekazana kuosha midumu na vyungu, na mapokeo, hivi kwamba walishindwa kuona Neno limefanyika mwili.

<sup>78</sup> Imejirudia. Imejirudia tena. Historia inajirudia yenyewe mara kwa mara. Naam, yeye alijua ya kwamba alikuwa na—Yeye alijua kuhusu Uzima, lakini Nikodemo hakujuua ya kwamba Yeye alikuwa ni Uzima. Hivyo ndivyo ilivyo leo. Watu wengi sana wanajaribu kumfanya Yesu, loo, Mwalimu mkuu, hata wanajaribu kusema Yeye alikuwa ni Nabii. Lakini unapojaribu kusema Yeye alikuwa ni Mungu, hilo limezidi kiasi. Unaona? Lakini Yeye alikuwa ni Mungu, na Yeye ni Mungu, na daima atakuwa Mungu. Hivyo tu. Hiyo ni kweli.

<sup>79</sup> Angalia, Yeye hata hakumwambia Nikodemo, sasa, wakati alipomjia, Yeye hakusema kamwe, "Sasa, Nikodemo, ninaheshimu sana, kwamba wewe ni mwa—mwa—mwalimu katika Israeli. Nitakwambia la kufanya, unatafuta Uzima wa Milele, labda inakubidi kuongezea elimu yako. Hutamki maneno yako sawa sawa," (upuuzi!) "ama labda unapaswa kushindania cheo cha juu zaidi katika madhehebu yako, ili upate Uzima wa Milele.

<sup>80</sup> Hivyo ndivyo watu wengi sana wanavyojaribu kufanya siku hizi, a-ha, cheo cha juu zaidi, wanataka watoke kuwa m—mchungaji wakawe mzee wa jimbo, ama—ama askofu fulani ama kitu kama hicho. Hilo halina uhusiano wo wote na Mungu.

<sup>81</sup> Angalia alichofanya mbele ya mtu kama huyo. Alimkemea kwa kutokujua saa aliyokuwa anaishi, "unataka kuniambia Mimi ya kwamba wewe ni mwalimu katika Israeli wala huwezi kufahamu mambo haya, wakati," Yeye akasema, "mtu hana budi kuzaliwa mara ya pili?"

<sup>82</sup> "Mbona," akasema, "mimi mzee, niingie katika tumbo la mama yangu?"

<sup>83</sup> Yeye akasema, "Na wewe ni askofu, kadinali, mzee wa jimbo katika kanisa la Kipentekoste," ama mtu fulani mwingine, "jamaa fulani mashuhuri katika madhehebu, wala hujui Maandiko?"

"Loo, tuna Musa."

<sup>84</sup> "Kama mngalimjua Musa, mngalinjua Mimi, kwa maana yeye ndiye aliyenena habari Zangu." Mnaona? Lakini si kulingana na mapokeo yao, madhehebu ya—yao, hilo lilikuwa ni tofauti. Lakini Musa kweli alinena habari Zake, Naye Ndiye Musa alinena habari Zake, na hata hivyo wao hawakujua jambo hilo. Kwa nini? Wao walijifunga sana na mapokeo, hata hawakujua jambo hilo.

<sup>85</sup> Na ndugu zangu wanaosoma, wanaochukua kanda hii, msizime sasa. Hebu na kidogo, hebu tuliangalie jambo hili waziwazi sana. Ninakupenda, wewe ni mchungaji. Wala mimi sijaribu kuwa mjuvi. Kama ninatoa mawazo hayo, basi simamisha kanda unionbee. Ninajaribu tu kukuletea jambo fulani ambalo ni Kweli. Usiliache likupite.

<sup>86</sup> Sasa, ninaheshimu utaratibu wa mwanadamu, na kadhalika, lakini mnapoyaunda haya madhehebu... Waangalieni Mafarisayo, hawakuwa na uhusiano wo wote na Masadukayo, kwa sababu Masadukayo hawakuamini aidha katika—katika malaika ama—ama roho, ama uufuo, wala cho chote kile, nao Mafarisayo waliamini yote mawili, nao walikuwa wanapigana vita. Sasa wa umoja wanaamini jambo moja, wa utatu wanaamini lingine, na Mmethodisti lingine, na Mpresbiteri lingine, nanyi mnawewekeana mipaka midogo midogo. Ndipo mna kitu gani? Utengano wa undugu. Jambo lingine, tutapata mahali

hapo katika Biblia katika muda kidogo tu, kwamba ni kitu gani, na kwamba Mungu anasema ni kitu gani.

<sup>87</sup> Sasa, la, Yeye hakumwambia kamwe aongeze elimu. Yeye alikuwa tu anamkemea kwa kutojua jambo halisi. “Je! wewe u mwalimu katika Israeli, na mambo haya huyafahamu? Ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, wala hamwezi kuyasadiki...” Wazia! “Mwalimu, cheo cha juu katika kanisa lenye kweli, askofu, kadinali, wala huwezi kufahamu mambo machanga ya kawaida ninayokwambia, utafahamu wapi mambo ya kiroho yanayotoka Mbininguni?”

<sup>88</sup> Lakini mzee mvuvi mbumbumbu ambaye hakuweza hata kuandika jina lake mwenyewe, alifahamu jambo Hilo, unaona, na aliwekwa kiongozi wa kanisa huko Yerusalem, Petro. Unaona? Loo, “Wote alionipa Baba, yeye atakuja kwangu.” Unaona? Wanaona jambo Hilo. Wanaliatkeleza, wakijua hakuna kitu kitakachowazuia.

<sup>89</sup> Ni kama tu yule mkulima. Si vizuri kufanya utani, bali ni kutoa mfano. Walisema mkulima aliatamisha kuku, wala hawakuwa na mayai ya kutosha, akaweka yai la bata chini yake. Wakati maskini bata mdogo alipoanguliwa, alikuwa kitu cha kuchekesha sana vifaranga wa kuku walichopata kuona. Alikuwa na uso mrefu wa kuchekesha, na alienda zake akilia kama bata kwenye eneo la ghala ya shamba badala ya kulia kama kuku, na—na hao kuku wote walikula na kudonoa ghalani. Na hicho hakikuwa chakula chake, hasa. Kwa hiyo siku moja maskini mama kuku akampeleka nje nyuma ya ghala, akashike panzi, na huko juu ya kilima kulikuwako na zi—ziwa. Na ikawa kwamba upepo ulipanda ukaja kutoka ziwanu, ndipo akisikia harufu ya maji. Ndiyo asili yake tu. Maskini mama kuku akasema, “Ku, ku, ku, ku, rudi!”

<sup>90</sup> Yeye akasema, “Kwak, kwak, kwak,” moja kwa moja kuelekea majini. Kwa nini? Yeye alikuwa ni bata, kwanza. Haidhuru huyo kuku alitta mara ngapi, yeye alikuwa bado ni bata.

<sup>91</sup> Na hivyo ndivyo ilivyo kwa mwanadamu ambaye amechaguliwa tangu zamani apate Uzima wa Milele. Wakati anapoona ile Nuru ya Mungu, hakuna madhehebu ya kutosha duniani ya kumwita ayarudie. La. Kwa nini? Ni asili yake. Huenda ikawa alikuwa akila nao kwa muda mrefu, na kula takataka zao na kujumuika, lakini anafikia mahali ambapo amepata jambo fulani tofauti, kwa hiyo yeye anajua jambo hilo. “Kondoo Wangu wanajua Sauti Yangu,” kasema Yesu, “mgeni hawatamuata.” Inawezekana wanafuata jambo fulani la kigeni, lakini ndani yao kuna kitu tofauti. Hebu wasikie Kweli siku moja, na uwaangalie. “Wote alionipa Baba watakuja.”

<sup>92</sup> Naam, Yeye alimkemea kwa kutokujua. “Wewe u mwalimu katika Israeli wala mambo haya huyafahamu? Huna budi

kuzaliwa mara ya pili!” Sasa, mtu wa kawaida, ninataka kuninii...ninyi mwone jambo fulani hapa, “Huna budi kuzaliwa mara ya pili.”

<sup>93</sup> Sasa, maisha ya kawaida, kama tuna maisha ya kawaida, ili kuwa hai katika maisha haya ya kawaida, katika mambo ya kawaida, hatuna budi kuzaliwa kawaida. Wao hawakung’oi tu kutoka kwenye mti fulani mahali fulani, unaona, wakakuweka huko kwa njia fulani. Walijaribu jambo hilo, lakini halikufanikiwa. Haina budi kuwa ni kuzaliwa halisi, kuzaliwa kwa kawaida, kukufanya mtu hai ili uwe na zile hisi tano, kutembea, kuongea, kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia, kutembea, na kadhalika, kwa sababu basi wewe ni mwanadamu, na una—unapasiwa mambo haya yote kwa maana yanaingia kwenye maisha ya kawaida.

<sup>94</sup> Na, katika kuzaliwa kama huko, mara nyingine tunakuwa werevu sana katika hekima ya ulimwengu ama mambo ya ulimwengu, tunakuwa Marais na—na wasomi maarufu, na mafundi stadi na wanasayansi, na kadhalika. Nanyi daima mnajua, tangu hapo mwanzo kabisa, watoto wa Kaini ndio waliokuwa na hekima ya namna hiyo; si wa Sethi, wao walikuwa wachunga kondoo wanyenyeketu. Lakini watoto wa Sethi walikuwa watu wacha Mungu. Lakini watoto wa Kaini daima walikuwa werevu, wakubwa, sayansi, madaktari na watu mashuhuri. Hiyo ni kweli. Biblia ilisema hivyo, mwajua, Hiyo inafundisha hivyo. Na wa dini sana, bali hatimaye waliangamia. Tunakuwa wenye hekima kwa kwenda shulen, kuchukua utaalamu, na kadhalika, tunakuwa wenye hekima sana, werevu, na tunaweza kufanya mambo na kusema mambo, na mara nyingine tunamshinda kwa maneno mtu aliyejazwa na Roho. Je! Yesu hakusema, “Wana wa ulimwengu huu ni wenye hekima kuliko wana wa Ufalme”? Hakika, maana wao, kwa hekima yao kwamba wanaweza—wanaweza kuzungumza na kuwashinda akili na kuwashinda maneno, na kuchukua Maandiko na kuyageuza na kuyafanya yaseme mambo ambayo hayasemi.

<sup>95</sup> “Loo, hayamaanishi hivyo hasa.” Mtu anaposema jambo hilo, mkimbie. Mungu hulinda Neno Lake, mwajua, Biblia ilisema. Limeandikwa jinsi tu linavyopaswa kuandikwa. Unaona? Sasa, yameewekwa namna hiyo yapate kudanganya, ama kuwafanya wenye hekima wakwazwe Nay. Ni rahisi sana, hiyo ndiyo sababu wao wanajkwaa kwake. Mnaona? Vema.

<sup>96</sup> Wanaweza kukusanya hekima hizi zote na kadhalika, bado, lakini vinatoka...kuzaliwa huko kunatoka chini, dunia hii. Ni kwa dunia hii, na kunapingana na Roho wa Mungu. Kuzaliwa kwa kwanza, kutufanya hai hapa, kunatufanya mwanadamu, kwa sababu ya tendo la dhambi kule kwenye ile bustani, kulimfanya mwanadamu kuja ulimwenguni kwa njia ya mwanamke. Na mwanamume aliyezaliwa na mwanamke ni

wa siku chache, lakini mwanamume aliyezaliwa na Kristo ni wa Milele. Ayubu alisema, "Mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke siku zake si nyingi naye amejaa taabu." Angalia, lakini mtu aliyezaliwa na Kristo, hana budi kuzaliwa kutoka Juu. Sasa, lakini mwanadamu aliyezaliwa na dunia, anakuwa mwerevu na karibu anaweza kumshida akili.

<sup>97</sup> Angalia jinsi Ibilisi alivyokuwa mjanja, alipumbaza kila kuhani aliyekuja duniani. Hakika alifanya hivyo. Alipumbaza, angali anafanya jambo hilo. Naam, hakika alifanya. Alikuwa mwerevu, lakini alikutana na mshindani wake, siku moja, Ambaye alimshinda. Na jambo pekee litupasalo kufanya ni kumkabili tu, Yeye amemshinda tayari. Unaona?

<sup>98</sup> Lakini ni kutoka chini, nao, hekima hii ambayo mwanadamu hutapa kuthibitisha na kuonyesha mambo haya yote kwamba ni kwa nini mtu afanye jambo *hili* na mwanadamu afanya *lile*, ni kinyume na ni uadui (akili za kimwili) kwa Mungu. Maandiko yalisema hivyo. Kweli. Haidhuru ni mwerevu jinsi gani, wanavyoweza kuligeuza. Ninataka mtu anionyeshe mahali ambapo Mungu alipata kuwa na madhehebu ama aliwahi kuongoza moja, ila kwamba anayahukumu hapa katika Biblia. Haidhuru wanawenza kujaribu kuwa werevu namna gani, ni kinyume! Jinsi hekima inavyoweza kusimama na kukushinda katika mabishano, na kukufanya ujisikie mdogo namna *hiyo* kwa kukwambia habari zake, lakini ni kinyume cha Maandiko.

<sup>99</sup> Mtu fulani aliniambia, "Ndugu Branham, kuna jambo moja niko kinyume nawe." Kasema, "Wewe ni Yesu Pekee."

Nikasema, "La. Mimi si mfuasi wa madhehebu yo yote."

<sup>100</sup> Mzee wa mkoa fulani alituma, hivi majuzi, na kusema, "Mtu fulani aliniambia wewe ni Yesu Pekee, Ndugu Branham."

Nikasema, "Huo ni uongo. Hiyo si kweli."

<sup>101</sup> Kasema, "Waliniambia ya kwamba wewe unaamini katika mapenzi huria, ya kwamba wanaume wanaruhusiwa kuacha wake zao na kutafuta..." Sasa, unaona, huo ni uongo tu wa Ibilisi. Mnajua hivyo.

<sup>102</sup> Nikasema, "Mimi ninapinga kwa dhati mambo kama hayo yasiyo ya kimaandiko! Ninaamini katika utakatifu na usafi. Ninaamini ya kwamba mwanamume amefungwa kwa mke wake mradi tu wakali hai." Haikupasi kumchukua bila kuomba kwanza.

<sup>103</sup> Na Yesu Pekee, kundi la Yesu Pekee, sina kitu dhidi yao, wao ni wazuri tu kama kundi lo lote lile, kwangu mimi. Lakini wanabatiza makosa, wanabatiza kwa kuzaliwa mara ya pili. Ninaamini ya kwamba tunazaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, si kwa maji. Ninatumia Jina la Yesu Kristo katika ubatizo, na hakuna Andiko lingine katika Biblia kuunga mkono...kulipinga. Hakuna mtu katika Biblia

aliyepata kubatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Ninataka mtu fulani aje anionyeshe mahali pamoja mtu mmoja alibatizwa namna hiyo. Basi, kama si la kimaandiko, acha kulifanya!

Unasema, "Haileti tofauti yo yote."

<sup>104</sup> Ililetä kwa Paulo. Yeye aliwaamuru kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo, halafu wampokee Roho Mtakatifu. Na Paulo alisema, "Kama malaika kutoka Mbinguni," Galatia 1:8; "akija, afundishe Injili nyingine," mbali na ile yeye aliyoukuwa amefundisha, "na alaaniwe."

<sup>105</sup> Unaona, ni mapokeo. Nilizungumza na mtu mmoja mashuhuri hazijapita siku nyingi. Kasema, "Ndugu Branham, siwezi. Ninajua Hiyo ni kweli," akasema, "lakini nifanye nini kuhusu hilo?"

Nikasema, "Litii!"

Akasema, "Mbona, ni—nina sifa mionganoni mwa watu."

<sup>106</sup> Nikasema, "Lakini mimi ninataka sifa kwa Mungu, kwa hiyo tii Neno Lake. Huna budi kujichagulia, je! utamtumikia Mungu ama mwanadamu?"

<sup>107</sup> Lakini wanapata madhehebu yao, wanaweka matangazo haya ndani yake, wanafuata moja kwa moja. Mara ya kwanza hilo lilipata kutumiwa ilikuwa katika kanisa Katoliki la Kirumi. Hiyo ni kweli. Ninataka mtu fulani atakayenionyesha jambo fulani kinyume na hilo. Ninasoma historia, pia, mwajua. Kwa hiyo, kumbukeni, huo ni ubatizo wa Kikatoliki, na kila mtu ambaye anabatizwa namna hiyo anabatizwa katika ushirika wa Kikatoliki. Nitathibitisha jambo hilo kabla usiku haujawkisha, Bwana akipenda. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu hamna budi kurudi.

<sup>108</sup> Si Yesu Pekee. Sasa, kuna watu wengi wazuri katika kanisa la Yesu Pekee. Watu wengi wazuri katika Assemblies of God, Church of God, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, na Katoliki. Lakini hakuna moja la hayo ambalo ni Kanisa, hakuna hata moja la hayo. Kuna watu binafsi mle ndani walio wafuasi wa Kanisa. Lakini si madhehebu hayo waliyo nayo ambayo huwafanya Kanisa, kama vile wanadamu wanavyojaribu kulifanya hivyo. Ni kosa. Hebu kidogo tuendelee kuwapa baadhi ya Maandiko katika muda kidogo.

<sup>109</sup> Naam, kuwa hai duniani, huna budi kuzaliwa kwa kawaida upate kuwa hai, na kuzaliwa kama huko hutufanya werevu kama nilivyosema. Unaona? Nasi tunakuwa werevu, wenye akili, akili zetu hutupa hiyo. Lakini kumbuka ya kwamba kuzaliwa huko, chanzo chake kabisa, ni jambo lililo kinyume. Ni la duniani na ni kinyume cha Neno la Mungu, upumbavu kwa Mungu na kwa mpango Wake, hakuju i mpango wa Mungu. Kama haikuwa hivyo, Nikodemo angalijua zaidi ya Yesu alivyojua juu ya jambo

Hilo. Unaona? "Je! wewe u mwalimu katika Israeli?" Unaona? Unaona mahali madhehebu yenu yanapokwenda, mahali watu wenu wakuu na wenye akili wanaokutanika pamoja na kupanga mipango yao, na kuketi?

<sup>110</sup> Hebu niwaambieni jambo hili. Kila wakati Mungu anapotuma Nuru duniani, juu ya jambo fulani kwenye Maandiko, wanaliendea harakaharaka moja kwa moja. Na mara mtu huyo anapoondoka, wao wanaunda madhehebu kutoka kwake. Na mara wanapounda madhehebu ya hiyo, nataka kumwuliza mwanahistoria ye yote (aliyepo hapa sasa hivi, ama aliye kwenye kanda) aje anionyeshe. Wakati wo wote ambapo mtu alipata kuunda madhehebu ya kanisa, lilikufa papo hapo wala halikuinuka tena. Ni kinyume cha Mungu. Ni kinyume cha Maandiko. Kwa hiyo mimi ninayapinga, cho chote anachopinga Mungu. Kama Mungu yumo ndani yangu, basi mimi ninapinga kile Mungu anachopinga. Adui wake ni adui wangu. Kanisa Lake ni Kanisa Langu. Uzima Wake ni Uzima wangu. Yeye alitoa Uhai Wake, alifanyika mimi kusudi mimi kwa neema Yake ninaweza kuwa kama Yeye. Unaona? Tulibadilishana nafasi zetu. Alifanyika mwenye dhambi kama mimi na akafa kwa ajili yangu, mahali pangu, kusudi nipate kuwa mwana wa Mungu kama Yeye alivyokuwa.

<sup>111</sup> Sasa unaona mahali madhehebu yenu yamefikia tayari? (Hatujaanza.) Werevu katika hekima ya kilimwengu lakini wafu kwa mpango wa Mungu! Sasa hebu na turudi nyuma, tusimame hapa kwa muda kidogo tu.

<sup>112</sup> Adamu alikuwa kinyume cha mpango wa Mungu, maana alikuwa ameasi Neno. Alijaribu kujifanyia kifuniko, dini. Ikashindikana, na daima limeshindikana, kile mtu anachojaribu kufanya. Nimrodi alikuwa amekosea. Kora aliangamia. Walikuwa wakijaribu kufanya nini? Kufanya madhehebu.

<sup>113</sup> Na baada ya jambo hilo, wakati hatimaye walipojiundi madhehebu, Yesu alikuta, wamekufa! Kasema, "Mna macho wala hamwon. Mna masikio wala hamwezi kusikia." Mnaona? Kasema, "Ninyi ni vipofu, mnaowaongoza vipofu. Kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, wote wawili si wataanguka shimonii?" Yeye akasema, "Wewe u mwalimu katika Israeli, na huwezi hata kufahamu kuzaliwa upya ni nini? Ambapo, kama ungalikaa mbali na hayo mapokeo, na kulishikilia Neno, ungalijua ya kwamba nilikuwa ninakuja kumpa mwanadamu uzao mpya. Ungalijua siku Yangu. Kama ungalimjua Musa, ungalinjua Mimi. Musa alinena habari Zangu na alisema kwamba nitakuja, nami Niko hapa nimewasili! Na kama sifanyi mambo ambayo Musa na manabii walisema ningefanya, basi msiniamini. Kama sizifanyi kazi za Mungu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama hamwezi kuniamini, nikiwa Mwanadamu, na kama hamwezi kuniamini kwa sababu Mimi ni Mwanadamu

na ninazifanya kazi za Mungu, aminini hizo kazi kwa kuwa zinashuhudia kazi ninazofanya Mimi.” Unaona?

<sup>114</sup> Lakini basi, kama ilivyo leo, kama Yeye angalikuwa ameishi duniani leo, Waassemblies of God wangekuwa na mmoja, wa Umoja wangekuwa na mmoja, na kila mtu angekuwa na Yesu fulani. Hakika, madhehebu yao yabidi yawe ndiyo yaliyo na mpira. Unaona? Kama mpira hausongi mbele, basi wao si wakweli. Kutenganisha undugu.

<sup>115</sup> Ninamkumba mvulana mdogo aliyeitwa “Daudi Kadogoo.” Yeye ni mwanamume, ameoa sasa, nadhani ana familia. Ninakumbuka wakati alipoanza mara ya kwanza. Nilienda St. Louis. Nimesikia habari za wavulana wadogo wahubiri, ambapo angepanda kule na kusema, “Yesu, mvulana mdogo, aliyezaliwa katika hori. Mama, hiyo hadithi inaendeleaje?” Lakini si mvulana huyo mdogo. Alitupa koti lake, akachukua fungu la maneno na kuhubiri. Lakini ye ye aliwa nini? Ilitokea kwamba yeye ni mfuasi wa Yesu Pekee. Baba yake, Bw. Walker, alikuwa mfuasi wa Yesu Pekee. Mbona, Waassemblies hawangeweza kustahimili jambo hilo. Iliwabidi kujitafutia Daudi kadogoo. Mbona, wengine iliwabidi wajipatie na wao Daudi kadogoo. Na wakati mmoja wakati mvulana huyo mdogo alipokuwa akifanya mukutano huko Florida, aliniita nije nimsaidie. Na mimi pamoja na Ndugu Moore tukasoma kurasa mbili za sehemu ya mbele ya gazeti, ambazo hazikuwa na kitu ila akina Daudi kadogoo, kila kanisa lilikuwa na Daudi kadogoo. Loo, jamani! Mbona, kama kundi la wazee wa Mungu wangalikitambua kile kipawa katika jamaa huyo mdogo, yeye angalizoa maelfu ya watu kuingia katika Ufalme, unaona, mpaka asahau mapokeo yake kuhusu mtu na mambo kama hayo. Mungu alikuwa na kipawa katika maisha yake, alikitumia.

<sup>116</sup> Wakati kuponya Kiungu kulipoletwa kwa mara ya kwanza, kila mtu alikuwa na hisia fulani mikononi mwao na wangeweza kunusa harufu ya magonjwa. Loo, jamani! Mbona? Iliwabidi wafanye jambo hilo, madhehebu yao yalikuwa yameachwa nyuma. Unaona, mmeweka madhehebu yenu mbele ya mpango wa Mungu, mnafikiri ndio huo. Lakini Mungu analijalia Kanisa Lake kuendelea mbele hata hivyo, Mwili wa kisiri. Hujiungi na Huo, unazaliwa Humo.

<sup>117</sup> Werevu katika hekima ya ulimwengu, lakini wamekufa katika mipango ya Mungu. Niambieni, basi. Niambieni, basi. Unaweza kuwaambia na kuwathibitishia ya kwamba wote wamekosea, kwa Neno la Mungu na ahadi Yake, na hata hivyo hawataona jambo hilo. Nawenza niketi chini na kuchukua Neno na kuwaonyesha ya kwamba madhehebu si kitu halali. Ninaweza kuwaonyesha ya kwamba kanuni za imani mlizo nazo siku hizi si halali, mnaona, kanuni hizi za imani za kanisa. Niwaonyeshe kwamba si halali, nao watasema, “Vema, tumefundishwa kuamini jambo *hili*.” Mnaona, nionavyo mimi,

ni—ni takataka, kama mnajua ninalozungumzia, chakula cha mzinga. Naam, hiyo ni kweli. Hawawezi kuona. Yesu alisema, “Ninyi, ha—hamwezi kuona, mpate kuja Kwangu mpate Uzima.”

<sup>118</sup> Kulikuwako na Nikodemo, mtu mwenye kuheshimika, mtu mashuhuri, askofu katika kanisa lake, mtu mashuhuri, aliyependwa na kila mtu, naye alikuja kwa Yesu naye hakuju mengi zaidi juu ya uzima kuliko—kuliko kitu cho chote kile. Yeye alikuwa mjinga sana kwa jambo Hilo wakati Yesu alipomkemea kwa ajili ya jambo hilo, lakini yeye alikuwa mwaminifu vya kutosha kuja. Hao wengine wote hata hawangeweza kuja. Walisimama mbali pamoja na kuhanini mkuu pamoja na Askofu *Fulani* na *Fulani*. Mnaona? Walisimama mbali pamoja nao, wakiona afadhali wachukue mapokeo ya wazee wao kuliko kusikia Neno la Mungu.

<sup>119</sup> Sasa, unawenza kuwaambia, hawatasikiliza. Unawenza hasa... Ungeweza kuwazia... Ninataka kuwaauliza jambo fulani. Sina maana ya kukufuru kwa jambo hili. Sasa, Ndugu mnaosikiliza kanda, sina maana ya kukufuru kwa jambo hili. Mngeweza kuniwazia mimi nikitoka nje hapa nje, na—na fundo mtini lingeweza kuniuliza, “Unawezaje kutembea kila mahali jinsi unavyofanya? Nina uhai, mimi ni fundo kwenye mti huu”? Yeye anawenza kuthibitisha ya kwamba ana uhai, lakini ni wa aina mbaya. Kama anataka kutembea kila mahali, jinsi tu anavyoweza kutembea kila mahali, kuona, kuonja, kugusa, kunusa na kusikia, kama angeweza kuzungumza na kuniambia na kuuliza jambo hilo, njia pekee, ingembidi kuzaliwa vile vile nilivyoziyalwa. Amina. Hataweza na kuelewa na hilo kwa njia nyingine yo yote. Lakini kama amezaliwa sawasawa na nilivyoziyalwa, basi yeye atajua mambo yale ninayoyajua mimi. Amina. Loo, jamani! Naam, bwana. Huwezi kuliambia fundo mtini jinsi tunavyotembea na kutenda hili na lile, itabidi lipokee uhai kama wetu lipate kufahamu. Ndivyuo ilivyo na Roho! Ni jambo lile lile na Roho, la sivyo huwezi kufahamu Hilo. Hakuna haja ya kujaribu kuwazia jambo Hilo zima, wewe njoo tu Kwake kwanza. Kwa kuwa, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezি hata kuuona Ufalme,” Yeye alisema, hiyo ni kusema, “kuufahamu.” Huna budi kuzaliwa mara ya pili kusudi upate kuujua Huo.

<sup>120</sup> Vema, unasema, “Mimi nimezaliwa mara ya pili.” Na unakana Neno? Unawezaje kuwa umezaliwa mara ya pili? Maisha yako mwenyewe yanakupa thibitisho lake, kundi lako mwenyewe ambalo umejiunga nalo, kila ndege na wimbile. Unaona? Ngoja mpaka tutakapoyafikia mambo hayo mnamo dakika chache, unaona.

<sup>121</sup> Linakuja kwa Roho. Unawezaje kuwaambia watu mambo ya Roho ambao hawajazaliwa kwa Roho? Huna budi kuzaliwa kwa Roho kufahamu mambo ya Roho. Ninii... Yesu alisema, “Upepo huvuma upendako, wewe huwezi kujuua unakotoka wala unakokwenda.” Unaona? Kadhalika na hali yake kila mtu

aliyezaliwa kwa Roho, hawawezi kujua. Mtu aliyezaliwa kwa Roho hafikirii, ye ye humwacha Mungu afikirie.

<sup>122</sup> Unafikiri ningeweza kusimama jukwaani hapa, niwazie na kumwambia mtu fulani kule nyuma, "Jina lake ni *John Doe* na anatoka mahali *fulani*, amefanya *hivi*. Naye alioa mwanamke mwingine kule nyuma, na ni miaka ishirini iliyopita, naye alizaa watoto kwa mwanamke huyu. Hana budi kurudisha kitu *hiki*, na kufanya *vile*," unafikiri, kwa kuwazia, ningeweza kufanya hivyo? Hakuna hekima kama hiyo katika kuzaliwa hapa duniani kwa jambo hilo. Ni zaidi ya hiyo. Haina budi kutoka Juu. Ndipo wakati unapozaliwa kwa Roho, Juu, Uhai uliokuwa ndani Yake Yeye aliye fanya mambo hayo, aliye sema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya."

<sup>123</sup> Kuzaliwa kwako hakuna budi kubadilishwe. Umedanganywa. Huenda ulinen a kwa lugha, huenda ulirukaruka, huenda ulipiga makelele, huenda ulifanya haya *yote*, *yale*, na *mengineyo*, huenda ulikuwa mfuasi mwa—mwaminifu. Vivyo hivyo na Nikodemo naye, unaona, lakini hakuwa amezaliwa. Na wakati unapolikana Neno, kujaribu kuliweka mahali pengine na ufanye jambo fulani Kwake, na kulisambaza namna hiyo. Basi Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Mradi tu Injili inahubiriwa, ishara hizi zitafuata. Niambie mahali ambapo aliwahi kuliondoa kutoka kwenye kanisa. Nionyeshe Andiko ambapo alisema, aliwahi kusema, "kwa kipindi fulani tu." Alisema, "Ulimwenguni kote na kwa kila kiumbe!"

<sup>124</sup> Naam, ingekubidi kupokea aina ya Uhai kama aliokuwa Nao, kusudi upate kuiishi Maisha Yake. Na unapoona Maisha Yake, ndipo utajua Neno Lake. Hiyo ni Kweli. "Wakati Yeye," kijina cha kumtaja mtu, si wazo, si mawazo, si mwamsho, lakini "wakati Yeye, Roho Mtakatifu, atakapokua, Yeye atachukua mambo haya ambayo nimewaambia, na kuwafunulia, na mambo yajayo atawapasha habari zake." Huko ni kuzaliwa. Hiyo ni thibitisho ya kwamba ni Neno. Na wakati mtu anaposema ya kwamba ana Roho Mtakatifu, na anakana Neno la Mungu na kuliweka mahali pengine, Roho Mtakatifu anawezaje kukana Neno Lake Mwenyewe? Sasa nionyeshe madhehebu katika Neno. Haya basi. Unaona? Vema.

<sup>125</sup> Ungeweza kuwazia juu ya mfanyakia shara... Sasa huu ndio umbali ambao kanisa letu liko nyuma. Ungeweza kuwazia juu ya mfanyakia shara aliyeanza biashara hapa, na hapa pana... kwa kweli ni biashara inayofanikiwa, naye hana budi kupata msaada upesi sana, naye angeliendea kundi la watu waliokufa, mizoga, na kusema, "Mnaweza kuja kunifanya kazi?" Hawangemfaa kitu.

<sup>126</sup> Hiyo ndiyo sababu madhehebu hayainuki tena. Unaona? Kundi la wasioamini wakikusanyika pamoja kama Nimrod,

kama Korah, kama kote kote katika nyakati. Unawezaje... Yeye hakuyatumia kamwe, hajawahi kuyatumia madhehebu. Hawezi kufanya jambo hilo. Tayari liko nje ya mapenzi ya Mungu, yamepita hapo. Huwezi kuyafikia, huwezi kuyatafuta.

<sup>127</sup> Ungewezaeje kwenda kwa mtu ambaye hangeweza kusogea, kichwa, mkono na mguu vimepooza, umwambie ungetaka ashiriki kwenye mashindano ya riadha, apige mbio hizo kwa subira, awekee kando... Unaona? Angewezaeje kufanya hivyo wakati mtu huyo hawezi kusogea, amepooza? Huna budi kumwondolea kupooza, kwanza, ndipo aweze kupiga mbio.

<sup>128</sup> Hilo ndilo madhehebu yanayohitaji, kuponywa Kiungu. Loo, jamani! Ninatumaini sipati... sisikiki mkosoaji. Unaona, mimi sikosoi, lakini kama msumari haujapigiliwa, unang'oka kwa urahisi. Unaona? Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu hawezi kutumia madhehebu. Mara yanaponinii...

<sup>129</sup> Kumbukeni, ninaamini ya kwamba Martin Luther alikuwa na Roho Mtakatifu. Kweli kabisa. Labda si katika kiasi kilichoko sasa, kwa kuwa hakuwa ametolewa. Tumepitia mambo haya, ninyi watu wa maskani, hapa kwenye ubao. Lakini alimwamini Mungu, "naye aaminiye yuna Uzima wa Milele." Sikuwazia hata kidogo kwamba kuna mtu aliyeamini jambo hilo kama mimi, mpaka asubuhi ya leo, nilipomsikia Charles Fuller nilipokuwa nikishuka kwenda kule. Yeye anaamini, pia, ya kwamba kuzaliwa upya si ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kuzaliwa upya ni kuzaliwa. Roho Mtakatifu ni ubatizo. Unaona? Vema.

<sup>130</sup> Sasa tunaona ya kwamba mtu huyu hana budi kuzaliwa mara ya pili kusudi aishi na juhud. Vema, kuzaliwa kimwili, ndipo una hekima ya ulimwengu. Na hekima ya ulimwengu inamtii mwalimu wake wa kimwili. Kweli. Hiyo ndiyo sababu hasa ambapo mtu asiyezaliwa upya, na umwambie Neno la Mungu, wao watamwamini askofu wao, mzee wao wa jimbo ama madhehebu yao, badala ya Neno la Uzima. Kwa nini? Hajui kitu kingine cho chote ila hilo. "Ona sasa, mnajua, siku moja huenda nikawa mzee wa jimbo." Mbona, Nikodemo alikuwa mkuu. Hiyo hasa ilikuwa zaidi ya mzee wa jimbo, hiyo ilikuwa ni zaidi ya m—m—mchungaji, hiyo ilikuwa ni zaidi, huyo alikuwa mkuu katika Israeli. Unaona? Naam, naye alikuwa ni mtu mashuhuri, yeye alikuwa ni wa kundi hili wala hakujua cho chote juu ya Mungu hata kidogo. Unaona? Yote aliyojua yalikuwa ni historia fulani.

<sup>131</sup> Mungu wa historia ana faida gani kama Yeye si yeye yule leo? Mungu wa Musa ana faida gani kama Yeye si yeye yule leo? Mungu ambaye angeweza kumwokoa mtu msalabani ana faida gani kama hangeweza kumwoka mtu akiwa katika hali hiyo hiyo leo? Kama ninavyosema daima, "Inafaa nini kumpa ndege wako wa kurumbizi mbegu nzuri na vitamini, kumfanya apate mabawa mazuri na yenye nguvu na ya kupendenza, kisha unamweka kwenye kizimba?" Sielewi. Unajaribu kumwambia juu ya Mungu wa nguvu na kadhalika, na kumwingiza katika

madhehebu ambayo hata hayaamini katika kitu kama hicho. Unaona? Yote yako nje. Hiyo ndiyo sababu inashindwa, yeye amekufa. Huwezi kuyatumia. Mungu kamwe hakuyatumia.

<sup>132</sup> Wazia tu, Roho Mtakatifu kamwe hakutumia, kwa wakati wo wote, madhehebu, hakuna mahali po pote katika Maandiko ama hakuna po pote katika historia. Kama mtu ye yote kwenye kanda hii, ama aliyepo hapa, anaweza kunionyesha mahali ambapo Roho Mtakatifu alichukua madhehebu na kuanzisha ufuluo duniani, njoo uniambie. Ninataka uniambie limetoka kwenye kitabu gani cha historia. Unajua halimo katika Maandiko, kwa hiyo ninataka unionyeshe limetoka kwenye historia gani. Mungu kamwe hakutumia kitu kama hicho. Anamtumia mtu binafsi, daima.

<sup>133</sup> Vema, kuzaliwa kwa Roho. Sasa, kuzaliwa kwa mwili, na kuwa na hekima ya ulimwengu, hekima itamtii mwalimu wake wa kimwili. Kuzaliwa kwa Roho ni kuamini na kutii mafundisho ya Biblia, kwa Roho Mtakatifu. Na mtu aliyezaliwa kwa Roho atatii Neno la Mungu haidhuru mapokeo yo yote yanawambia nini. Ni hilo tu. Umezaliwa tena, hiyo ndiyo sababu unaona. Kuwa mfuasi wa madhehebu, kuweka matumaini yako yote katika hayo . . .

<sup>134</sup> Sasa, sisemi watu katika madhehebu hawajazaliwa mara ya pili. Sasa, nitaingilia jambo hilo mnamo dakika chache, Bwana akipenda. Hakika, wamezaliwa mara ya pili, lakini wao ni watu binafsi. Madhehebu siyo yamezaliwa mara ya pili; watu binafsi walio mle wamezaliwa mara ya pili. Lakini madhehebu humtenganisha tu na Mungu, hivyo tu ndivyo yanavyofanya, kumtenganisha. Vema. Bila kuangalia mwili, madhehebu hufundisha mambo ya mwili, daima ni kinyume cha mapenzi ya Mungu.

<sup>135</sup> *Kuzaliwa mara ya pili* kunamaanisha “kuzaliwa kutoka Juu.” *Mara ya pili* inamaanisha “kutoka Juu.” Nadhani unajua hilo, unaona. *Kuzaliwa mara ya pili* kunamaanisha “kuzaliwa kutoka Juu.” Sasa, utaona, unaweza kusoma jambo hilo ukitaka, kwenye kamusi. Unaona, kunamaanisha “kuzaliwa ambako kumetoka Juu.” Kwa sababu, umezaliwa *hapa*, sasa kuzaliwa mara ya pili huna budi kuzaliwa kutoka *Huku* juu, kuzaliwa mara ya pili. Basi Ufalme huo ni wa hali ya juu sana kuliko ufalme huu, ni wa hali ya juu sana kuliko ufalme huu, mpaka ufalme huu ni mpumbavu kwa Ule, na Ule ni mpumbavy kwa huu.

<sup>136</sup> Kama nilivyosema mara nyingi, mimi na mke wangu hapa si muda mrefu uliopita tulienda kununua vyakula, miezi michache iliyopita, ndipo tukamwona mwanamke aliyevaa sketi. Nalo lilikuwa ndilo jambo la kushangaza sana tulilopata kuona kwa muda mrefu.

<sup>137</sup> Vema, asubuhi ya leo, sisemi jambo hili kwa kukufuru, nilisikia moja ya mdhehebu makubwa yanayo julikana sana. Na mimi na binti yangu tulikuwa tukisikiliza redio tulipokuwa tunaenda kuweka kanisa fulani wakfu. Na wimbo walioimba, namna fulani ya kitu fulani juu ya mtu *Fulani*, baadhi ya huko kuimba bora kunakosikika kwangu kama kwamba ni wanawake wanaoshikilia pumzi yao mpaka uso unakuwa wa samawati, halafu wanafikiri ati huko ni kuimba. Huko ni kubweka. Mimi napenda kuimba kuzuri kwa kale kwa Kipentekoste, kunakotoka moja kwa moja moyoni mwako. Hungeweza kubeba tuni katika ndoo ya mkaa wa mawe, lakini hata hivyo unaimba, ukitoa sauti ya furaha kwa Bwana. Nafikiri hilo ni la kiroho. Ninalipenda. Lakini huko kushikilia pumzi yako mpaka uso unakuwa bluu, kisha inaisha halafu inarudi, ni nani... Hata wewe mwenyewe hujui unachoimba. Unatarajiaje mtu mwengine ye yote kujuua? Haya basi. Yesu alisema, “Tunanena mambo tujuayo.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Tunachopaswa kufanya ni kuimba kile tujuacho moyoni mwetu, kile tunachojisikia kuimba.

<sup>138</sup> Na wakati walipomaliza, binti yangu anajifunza muziki, naye alisema, “Ndugu,” akasema, “huo ulikuwa bora kweli.”

<sup>139</sup> Nikasema, “Ndiyo, lakini unafikiri ni wangapi kati ya kwaya hiyo ya kama watu hamsini walikuwa na harufu ya sigara? Unafikiri ni wangapi wa kwaya hiyo, jana usiku ikiwa ni Jumamosi usiku, hawakunywa pombe kidogo? Ni wanawake wangapi mle walikuwa wamekata nywele? Ni wangapi walikuwa wamejipaka rangi, wakati mchungaji wa kanisa hilo aliposema siku chache zilizopita, ‘Mungu aliumba ulimwengu mzuri zaidi wakati Yeye alipobuni vipodozi’”? Wakati, tunajua ya kwamba kuna mwanamke mmoja katika Biblia aliyejipodoa uso, ndipo Mungu akamlisha kwa mbwa. Nasi, mtu ye yote anayejua jambo lo lote juu ya kanisa na juu ya wagagani, anajua ya kwamba vipodozi ni alama ya upagani, imekuwa hivyo daima. Na, hata hivyo, wanawake wanajipaka. Na mwanamume akivuta sigara, akinywa pombe, akifanya yasiyofaa. Na kusimama pale na kuimba, sauti kama hizo. Tutafikia jambo hilo mnamo dakika chache papa hapa. Vema. Hayo ni mawazo ya kimadhehebu, wakati, kutakuwako na kuadhirkira kwenye ile Hukumu, nionavyo mimi.

<sup>140</sup> Kuzaliwa na Roho, ni kuamini na kuenenda katika Roho, ni kufahamu na kuamini kwa moyo wako ya kwamba Yesu ni Kristo na Hili ni Neno Lake, ya kwamba hakuna maneno mengine yanayoweza kuongezewa Kwake wala kutolewa Kwake bila ya jina lako kuondolewa kwenye Kitabu cha Uzima. Hilo lilikuwa kali. Kama ukiongeza jambo moja Kwake, katika mapokeo yako, ama uondoe jambo moja Kwake, vema, Kristo alisema, Yeye Mwenyewe, “Jina lako litafutiliwa mbali kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Sasa, tafuta shirika, madhehebu katika

Biblia. Utayatoroka! Vema. Bila kujali mwili, mafundisho ya madhehebu ni kinyume cha Biblia. Naam. *Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha* “Kuzaliwa upya kutoka Juu; kuzaliwa kutoka Juu.” Ndipo tunakuwa hai katika mambo yanayotoka Juu. Loo, jamani! Kwa kuwa ni Yeye Mwenyewe akitenda katika Neno Lake kuititia kwako, tawi Lake, kwa Mzabibu.

<sup>141</sup> Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini.” Loo, bila shaka! Yeye alisema, “Hakuna mtu aliyepaa Mbinguni ila Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni.” Mwangalie akimsahihisha Nikodemo hapa, wakati Nikodemo . . . Unajua, wao walifkiri, Yeye akiwa Mwanadamu, asingeweza kuwa ni Mungu. Naye akasema, na hapo akasema, “Hakuna mtu aliyepaa juu Mbinguni ila Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni, ndiye Mwana wa Adamu aliye sasa Mbinguni.” Hilo hakuweza kulistahimili. Angewezaje, Mwana wa Adamu, kushuka kutoka Mbinguni; kushuka kutoka Mbinguni, awe ndiye yeye yule aliyepaa kwenda Mbinguni; na ndiye yeye yule anayesimama hapa juu ya nyumba hii, akizungumza na Nikodemo, alikuwa Mbinguni sasa? Vema, alipaswa kuona ya kwamba ilikuwa ni Mungu. Yeye yupo kila mahali, kila mahali! Unaona? Lakini yeye, katika mapokeo yake, hakujuja jambo hilo. Hakuwa na nia ya kiroho. Nia ya kimwili, wala hangefahamu jambo hilo.

Anasema, “Watu husema kwamba Mimi Mwana wa Adamu ni nani?”

“Wengine husema, vema, ‘Yeye ni Mwana wa Daudi.’”

<sup>142</sup> Akasema, “Basi mbona Daudi katika Roho alimwita ‘Bwana,’ kusema, ‘Bwana alimwambia Bwana wangu, “Keti upande wa mconi Wangu wa kuume, hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu Yako”’?” Jinsi ambavyo Yeye alivyo Shina na Mzao wa Daudi pia; Yeye alimtangulia Daudi, alikuwa Daudi, na baada ya Daudi. Unaona? “Yeye ni Shina na Mzao wa Daudi,” Biblia ilisema hivyo, Shina na Mzao wa Daudi pia. Angewezaje kuwa Mwanawe basi? Angewezaje kuwa Bwana Wake? Biblia ilisema, “Tangu wakati huo hawakumwuliza kitu.” Nafikiri lilikuwa ni jambo zuri, pia. Naam, bwana. Vema.

<sup>143</sup> Kuzaliwa mara ya pili kutoka Juu. Ndipo tunakuwa hai, tunaishi katika mambo ya kutoka Juu, na, kwa kuwa Uzima Wake u ndani yetu, ambao ni Neno Lake likidhihirisha Neno Lenyewe. Roho aliye ndani yenu ni Neno lililofanyika mwili ndani yenu. Roho hulijali Neno, na yuko hai katika kudhihirisha Neno.

<sup>144</sup> Sasa, Roho hajishughulishi katika madhehebu yo yote. Hana haja na kufanya madhehebu, kwa maana Roho Mwenyewe anapinga madhehebu. Madhehebu yanatafuta mambo ya kilimwengu, nia ya ulimwengu, na wanajenga mahekalu makubwa na vitu vilinavyong’ara, na madhehebu mkubwa

yanayong'ara, wahubiri walionolewa, na kadhalika namna hiyo, na watu wa tabaka bora sana walioko mjini. Ambapo, Roho anajaribu kupata miyo miaminifu ambapo Roho anataka sana kudhihirisha na kuthibitisha ya kwamba kila Neno la Mungu ni Kweli. Unawezaje, Roho anawezaje kufanya kazi katika madhehebu wakati yanakana, yanachukua kanuni za imani badala ya Neno? Haiwezekani. Kwa hiyo, unaona, yamekufa. Mungu haendi kwenye sehemu hizo kutafuta ninii Lake, kukiundi la watu wa kumfanyia kazi, maana tayari wamekufa. Wao ni wasioamini katika Neno, la sivyo hawangekuwa huko. Unaona? Sasa, tuko hai katika mambo yanayotoka Juu. Sasa, Roho hulijali Neno. Sasa, hiyo ni kweli, maana Roho hulipa Neno Uzima. Unaona? "Andiko huua; bali Roho huhuisha."

<sup>145</sup> Sasa, nilikuwa nikija leo, nikiangalia ile miti mikubwa na ya kupendeza kule msituni, vilima vikubwa, vyenye majani yasiyokauka, ya hudhurungi, na ya manjano hapa na pale. Nikasema, "Unajua hiyo ni nini?" Nikasema, "Ndiyo kwanza tuwe na mauti, na Mungu ametoa nje shada Lake la maua, akayaweka huko vilimani. Ni maua ya mazishi. Uhai umerudi mavumbini. Mungu ndio kwanza azike mbegu Zake kutoka kwenye maua na kadhalika, akazizika tena, na ndiyo tu amechanusha shada Lake la maua. Yeye anaangalia kote duniani kwa sababu ni maua ya mazishi. Lakini wakati jua litakapochomoza tena, mbegu hiyo itapata uhai tena." Amina. Vema.

<sup>146</sup> Roho anataka kuthibitisha Neno. Na kama ulikubali mapokeo badala ya Neno... Sasa, unasema, "Vema, tunaliamini lote, lakini, Ndugu Branham, ninajua hatuamini *Hili*." Basi papo hapo ndipo unaposimama.

<sup>147</sup> Kasisi fulani wa jeshi aliniambia wakati mmoja ya kwamba yeye... ya kwamba ka—kapiteni mmoja alisema, ama ninaamini ilikuwa ni meja, alisema, "Kasisi, nenda kule, kuna kapiteni anayekufa. Amepigwa kwa bombomu."

<sup>148</sup> Akaenda kule, na kapiteni alikuwa akitapatapa. Wakamburuza wakamwingiza kwenye hema ya Msalaba Mwekundu, ndipo akasema, "Kapiteni."

<sup>149</sup> Akainua macho yake kuititia katika mbubujiko wa damu, ndipo akasema, "Naam, bwana." Naye akasema, "Wewe ni kasisi."

"Naam." Akasema, "Unakufa, Kapiteni."

Akasema, "Ninajua."

akasema, "Je! wewe ni Mkristo?"

Akasema, "Nilikuwa Mkristo."

<sup>150</sup> Kasema, "Ulimwacha wapi, Kapiteni?" Akasema, "Utampata mahali pale pale ulipomwacha." Hakika.

Kapiteni akasema, "Siwezi kukumbuka."

<sup>151</sup> Yule kasisi akasema, “Heri ukumbuke, una dakika chache tu zaidi, jinsi unavyougu.” Mdomo ulikuwa unahangaika.” Mdomo ulikuwa wazi, damu inatoka mdomoni mwake na masikioni, na amejaajisasi za bombomu. Kasema, “Bora ufanye haraka, mapafu yako yanajaa.”

<sup>152</sup> Ndipo yule kapiteni akaanza kuwazia huku na huko, amelala pale akitapatapa. Tabasamu likatokea usoni mwake, akasema, “Sasa najua.”

Kasema, “Ulimwacha wapi? Anza pale pale.”

<sup>153</sup> Akasema, ““Sasa najilaza nipate kulala.”” Hapo ndipo alipomwacha, hapo ndipo anapompata.

<sup>154</sup> Wakati madhehebu yako yanapofundisha jambo fulani kinyume cha Neno, unamwacha papo hapo. Rudi moja kwa moja, kwa maana Yeye ana juhudhi katika kuthibitisha na kulifanya Neno hilo kweli. Hivyo ndivyo Yesu alivyokuwa, daima akifanya mapenzi ya Baba. Unaona? Vema.

<sup>155</sup> Kwa hiyo, unaona, ufahamu wa madhehebu ya Nikodemo haukuwa na maana yo yote kwa Mungu. Sasa, haidhuru kama alikuwa ni mtu mkubwa, kama tunavyosema, katika madhehebu, mkuu wa Israeli, kusoma kwake kote na kufahamu hakukumaanisha hilo [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] hapo aliposimama mbele za Kristo, alikemewa tu. Sasa, nadhani watu wote wanasma, “Baba mtakatifu, Nikodemo. Baba mtakatifu, Nikodemo. Tunakusujudu, bwana.” Lakini wakati Yesu, yeye alisimama mbele za Mungu, alimkemea kwa ujingga wake. Kwa hiyo, unaona vile yote hayo yote yanakoelekeea, sahau mambo hayo! Hima, tumwendee Mungu. Hiyo ni kweli. Vema.

<sup>156</sup> Wala ufahamu mkuu wa Kora haukumaanisha kitu, ama wa Adamu, kila mmoja akikana Ujumbe wa Mungu uliothibitishwa. Sasa hebu na tusikilize kwa makini sasa, tutaingia kwenye maji yenye kilindi mnamo dakika moja. Unaona, kila mmoja wao, sababu ya wao kupata shida, Nikodemo, Kora, Nimrodi, na kadhalika, ni kwa sababu hawakumtambua mjambe wa Mungu aliyekuwa na Neno lilothibitishwa la siku hiyo. Sasa, kila mtu anajua jambo hilo. Sasa, tungeweza kukaa kwenye jambo hilo kwa muda mrefu. Lakini Mungu anabashiri na kusema jambo fulani litatukia; mwanadamu anaunda madhehebu, anamweka mtu sawasawa kabisa. Waliamini kulikuwa na Masihi ajaye. Loo, hao Wayahudi, loo, jamani, hakika! Lakini Yesu alipokuja jinsi alivyokuja, wao walisema, “Huyo hawezu kuwa ni Yeye.” Wanashindwa kufahamu Neno. Sasa, Yesu hakuja kinyume cha Neno (sivyo?), lakini Yeye alikuja kinyume cha tafsiri ya Neno yaliyokuwa nayo madhehebu. Musa hakuja kinyume cha Neno, alikuja moja kwa moja kulingana na Neno; lakini Kora alishindwa kuona jambo hilo. Na huko nyuma kote kote imekuwa namna hiyo.

<sup>157</sup> Sasa angalia. Ujumbe huu wa siku hizi hauwezi kamwe kuwa ni kitu cha kusema “tuna Ukweli na tuna *hii, ile*,” hauna budi kuwa umetangulia kutabiriwa katika Neno Lake! Na halafu baada ya Neno kuleta, halina budi kuthibitishwa kwa Neno.

<sup>158</sup> Yesu alithibitishwa vizuri na Mungu, kwa Neno. Yeye alisema, “Kama mngalimjua Musa, mngalijua siku Yangu.” Manabii walinena vema juu Yake, manabii wote walisema vema alivyokuwa Yeye. Na hata hivyo liliwapofusha, hawakuweza kulifahamu. Mnaona? Lakini Yesu alikuwa . . . Sasa msininii . . .

<sup>159</sup> Ninataka kusema jambo hili kwa ajili ya kanda, na kwa ajili yenu, pia. Mnaona, mjumbe mwenye Ujumbe wa siku hii!

<sup>160</sup> Sasa, ukienda, Wasabato husema, “Tumelipata, adhimisha Sabato tu!” Hebu mnionyeshe jambo hilo katika Maandiko. Bibi Eddie Baker alisema alikuwa nalo. Hebu mnionyeshe. Mashahidi wa Yehova walisema walikuwa nalo. Hebu nionyesheni. Mnaona? Wamethodisti wanasesma wanalo. Hebu nionyesheni. Wabatisti wanasesma wanalo. Nionyesheni. Nionyesheni madhehebu yo yote. Ninawathibitishieni ya kwamba hayo, kila moja lao, liko nje ya mapenzi ya Mungu. Kila moja la hayo liko kinyume, yanafundisha mapokeo ya mwanadamu badala ya Neno la Mungu. Sijui moja ya hayo ambayo yangekubali mambo ambayo kweli yameandikwa katika Biblia jinsi yalivyoandikwa. Hiyo ni kweli. Lakini wakati mtu anapopita na kusema, “Nina Ujumbe wa siku hizi,” hana budi aonekane vizuri kwanza na iwe ametabiriwa kuja.

<sup>161</sup> Wakati Yohana Mbatizaji alipoenda kule, wao walisema, “Je! Wewe ni Kristo?”

Akasema, “Mimi siye.”

Kasema, “Wewe—wewe—wewe ni Eliya?”

Akasema, “Mimi siye.”

Akasema, “U nani wewe?”

<sup>162</sup> Aliweza kujitambulisha, alikuwa na Ujumbe wa wakati huo. Akasema, “Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, kama alivyosema nabii Isaya. Sasa, kama kuzaliwa kwangu na maisha yangu hayakulingana na jambo hilo, msi—msinipokee.”

<sup>163</sup> Wakati Yesu alipokuja, lilikuwa ni jambo lile lile, jambo lile lile. Mjumbe mwenye Ujumbe, hauna budi kuwa ni Ujumbe uliotabiriwa na Mungu. Na basi Mungu, akizungumza kupidia kwa mjumbe huyu, anathibitishwa kwamba ni Kweli. Mnasikia hilo? Mnalifahamu? Lifahamuni! Kwanza haina budi kuwa ni BWANA ASEMA HIVI, iliyotabiriwa. Na halafu huyo mjumbe mwenye huo Ujumbe, haina budi kuwa ni yale Mungu aliyosema yangetukia wakati huo.

<sup>164</sup> Hivyo ndivyo Musa alivyokuwa. Hiyo ndiyo sababu alianguka kifudifudi mbele za Mungu, na kusema, “Mungu, Wewe ulinituma.”

Akasema, "Jitenge na kundi hilo."

<sup>165</sup> Unaona ninalomaanisha? Hicho ndicho kitu ambacho daima kimevuruga akili za watu, kikawaondoa kwenye mapenzi ya Mungu. Sasa kumbukeni, itabiriwe na Neno Lake na kuthibitishwa kikamilifu na Neno Lake. Sasa, Yesu alisema, "Kama nisipozitenda zile kazi, zile za Mungu, basi msiniamini. Mnaona, kama nikikosa... Kasema, ni nani kati yenu anishuhudiaye kwamba nina dhambi? Ni nani kati yenu awezaye kunionyesha Mimi kwamba ni asiyeamini?"

<sup>166</sup> Nikodemo akasema, "Tunajua Wewe u nanii... Rabi, umetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu angaliweza kufanya mambo hayo isipokuwa Mungu yu pamoja naye." Unaona? Kwa hiyo ilionyesha ya kwamba alikuwa mwamini.

<sup>167</sup> Sasa, sisi tunaojua historia ya kanisa. Sasa vaeni kofia zenu za mawazo. Hatujachelewa bado, mnaona, kwa hiyo sikilizeni tu kwa makini sasa nami nitajaribu kuharakisha jinsi niwezavyo. Na—nataka... Sikilizeni kanda hii kwa makini. Sasa, mtu ye yote ambaye amewahi kusoma historia ya kanisa, anajua ya kwamba mara ya kwanza ambapo Ukristo ulipata kufanywa madhehebu, ilikuwa ni kanisa Katoliki la Kirumi. Sasa, kama kuna nyakati zo zote kabla ya hapo, ninataka mtu fulani alete historia hiyo na anionyeshe. Mimi ni rafiki msiri wa Paul Boyd, wanahistoria wengi mashuhuri. Kule kwenye chumba changu cha kusomea, nina kitabu kiitwacho *Kabla ya Baraza la Nikea*, *Baraza la Nikea*, *Waanzilishi wa Nikea*, yote ni maandishi matakatifu ya kanisa, niyajuayo. Nimeyasoma kwa miaka thelathini na mitatu, nikayachunguza. Kamwe hakujakuwa na madhehebu. Kanisa Katoliki ndilo mama wa madhehebu. Tunajua ya kwamba hiyo ni kweli. Kanisa halijawahi kamwe kuunda madhehebu kamwe, kufanywa madhehebu, mpaka kwenye kanisa Katoliki. Nalo neno *katoliki* maana yake ni "ya ulimwengu mzima." Nao wameunda dini ya kanisa la taifa, na kuisambaza kote katika milki ya Rumi, na ilikuwa imeeneea karibu se—sehemu zote za ulimwengu uliokuwa umetekwa wakati huo. Lilikuwa ndilo kanisa la taifa, na wale ambao hawakulitii waliuawa. Baraza la Nikea, siku kumi na tano za vita vya umwagikaji wa damu, wakati manabii halisi wa Mungu, wakati waliposimama pale kwenye ninii zile . . .

<sup>168</sup> Kanisa Katoliki, sababu ya kuanzishwa kwake, mbona, sote tunajua jambo hilo, nimelifundisha hapa. Jinsi, kwa kweli, Akila na Priska alikuwa ndiye mchungaji, Akila alikuwa mchungaji wa—wa kanisa la Kirumi. Wakati Roho Mtakatifu aliposhuka kwenye Pentekoste, alishuka juu ya Wayahudi waliotoka katika kila taifa chini ya mbingu. Lakini siku chache baada ya hapo, Petro aliona ono akiwa juu ya nyumba, kwamba aende kwa Cornelio, Mrumi, mtu mwenye haki, ndipo akaomba na Roho Mtakatifu akashuka juu yake. Baada ya kitambo kidogo watu mashuhuri wakaanza kulipokea. Akila na Prisila wa—wakaenda

Rumi nao wakaunda madhehebu, ama, hawakuunda madhehebu kamwe, lakini waliweka kanisa la kwanza la Rumi katika utaratibu. Ndipo, walipofanya hivyo, walikuwa na ndugu na dada za—zao.

<sup>169</sup> Naye Klaudio, katika utawala wake, aliwafukuza Wayahudi wote kutoka Rumi. Na huo ndio wakati ule ule ambapo kanisa Katoliki la Kirumi lilisema Petro alikuwa Rumi. Nionyeshe Andiko moja ambapo Petro alipata kuwa Rumi, ama historia yo yote inayosema alikuwa huko. Hakuwa huko, kulingana na Neno la Mungu, na Hilo ndilo ninaloamini mimi. Na Petro angeweza je, akiwa Myahudi, kuvumilia kamwe ibada za sanamu na upuuzi walio nao, wa kuabudu sanamu na kadhalika? Ambapo... Unaona? Angeweza je kupinga mafundisho yake mwenyewe hapa? Upuuzi. Hiyo si zaidi ya Waprotestanti walivyo pia. Ngogeni, tutalifikia jambo hilo baada ya kitambo kidogo, karibuni, Bwana akipenda. Angalia. Angalia sasa, tunaona ya kwamba wakati ule ule ambapo kanisa linasema Petro alikuwa Rumi, historia inasema kwamba Klaudio (na Biblia ilisema pia) alikuwa amewafukuza Wayahudi wote watoke Rumi.

<sup>170</sup> Ndipo Paulo akapitia Efeso na akaja kwenye pwani za juu kule, anawakuta wanafunzi hawa, naye alikuwa kule kumtembelea Akila na Priska. Baada ya wao kuondoka, ndipo ndugu wa Kirumi katika kanisa hili wakaanza kubuni mawazo yao wenyewe, ndipo wakaingiza ibada za sanamu. Na ndipo katika Konstantino, ambaye mama yake alikuwa ni Mkristo halisi na alitumaini mvulana wake angekuwa Mkristo halisi, bali alikuwa mwanasiasa. Naye aliona kwamba karibu Rumi yote, ama sehemu yake iliyo kubwa, ama, tabaka maskini tayari walikuwa wamekubali wokovu katika Kristo. Na ndipo wakaanza kupendwa sana na watu, kwa maana walikuwa wakimshusha Vinasi na kumwinua Mariamu, na kumshusha Jupita na kumwinua Petro, na kadhalika namna hiyo na—na hao wanafunzi, na ilikuwa ni dini iliyopendwa sana na watu. Nao walikuwa hodari. Wao, hao Wakristo wangekufa!

<sup>171</sup> Ndipo kanisa Katoliki likasema, “Sisi tulikuwa wa kwanza.” Hiyo ni kweli kabisa, kanisa Katoliki lilianza kwenye Siku ya Pentekoste. Lakini hili hapa jambo lililolitupa nje, liliunda madhehebu na kuingiza (kutoka kwenye Neno) mafundisho ya sharti. Na fundisho la sharti la sasa hivi, ninyi watu mlion na zaidi ya miaka kumi mnaweza kukumbuka lile fundisho la sharti hivi karibuni, ni kule kupaa juu kwa Mariamu, yapata miaka kumi iliyopita. Fundisho lingine la sharti lililoongezewa kwa kanisa. Badala ya Maandiko, ni fundisho la sharti! Nao watakuufahamisha sasa hivi, wao “hawajali vile Maandiko yasemavyo, ni yale kanisa lisemayo.”

Wao, yule kasisi aliniambia, kasema, “Mungu yumo katika kanisa Lake.”

Nikasema, “Mungu yumo katika Neno Lake.”

<sup>172</sup> Akasema, "Vema, Biblia hiyo ni historia tu ya kanisa Katoliki la mwanzoni."

<sup>173</sup> Nikasema, "Basi mimi ni Mkatoliki wa mwanzoni." Nikasema, "Hilo linanifanya Mkatoliki zaidi kuliko ulivyo wewe, ukiwa kasisi." Unaona? Nikasema, "Kama ndivyo ilivyo, basi mimi ni huyo." Nikasema, "Unaona, ninaamini vile hasa mitume walivyofundisha. Unaamini kile mwanadamu aalichoingiza ndani yake." Na hivyo ndivyo mambo yalivyoendelea hasa. Hakika, ilikwa hivyo. Ndivyo yalivyoendelea, namna hiyo kabisa.

<sup>174</sup> Sasa angalia historia. Ndipo wakaanza kuongeza mafundisho ya sharti, mafundisho ya sharti. Na wakati Paulo alipokuja, tunajua, kulingana na historia, ya kwamba hatu hakulitembelea kanisa hilo la kwanza, kwa maana asingeweza kuvumilia ibada za sanamu. Ndipo alilitembelea kanisa la pili ambalo walikuwa wamelianzisha, kanisa la pili la Rumi.

<sup>175</sup> Basi wakati hilo Baraza la Nikea lilipokuja, ambapo Konstantino aliona wazo la kuunganisha ufalme wake. Jambo lile lile Ahabu alilofanya na Yezebeli, kuoa kule. Unaona? Na hapo alipoona nafasi ya kuunganisha watu wake na kufanya taifa kubwa lenye nguvu kwake, alidhani wangepata dimi yao, kwa hiyo akawafanya dini ya kanisa la taifa. Basi wakati walipofanya lile Baraza la Nikea, na maswali haya yakazuka kama kulikuwa na Mungu mmoja, ama watatu; kama wanapaswa kubatiza katika Jina la Yesu Kristo, ama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu; maswali haya yote yalifikia kwe—kwenye shindano la kuamua humo. Na, wakati ilipotendeka, baadhi ya hao manabii wa kale wakatokea kule bila kitu ila ngozi ya kondoo waliyovaa, na wanakula mboga. Kweli! Lakini hao watu mashuhuri walikuwa tayari wamejipandisha vyeo kanisani, wakawanyamazisha kwa hekima ya kilimwengu. Lakini walikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Likaingia katika giza la upagani kwa kama miaka elfu moja.

<sup>176</sup> Lakini likatokea tena, kuchanua. Hiyo ni kweli. Huwezi kuliua. "Nitarudisha, asema Bwana, miaka yote vitu hivi vimekula."

<sup>177</sup> Hayo madhehebu yaliongeza fundisho la sharti. Na ili kufanya jambo hili, kuongeza fundisho la sharti, njia pekee ambayo kanisa lo lote, njia pekee ambayo madhehebu yo yote yanaweza kuacha Neno la Mungu, ni kuongeza fundisho la sharti badala ya Maandiko matakatifu, ni kujaribu kufanya mapokeeo yako ama mafundisho ya kanisa lako, ingawa ni kinyume cha Maandiko. Basi mnawezaje kulaumu kanisa Katoliki, wakati mnapofanya jambo lile lile walilofanya? Mnaelewa? Vema. Wakati, sasa wazia tu, Maandiko hayawezi kushindwa! Mafundisho ya sharti ni uongo, kwanza. Na wakati unapokubali madhehebu fulani, tayari una fundisho la sharti, kwa sababu

ni jambo fulani lililoongezwa. Halimo katika Maandiko. Halimo katika Maandiko.

<sup>178</sup> Hakuna kitu kama madhehebu. Yesu kamwe hakusema, “Ninawaagiza mwende ulimwenguni kote, mkaunde madhehebu.” La, bwana, hakuna kitu kama hicho! Kufanya jambo hili, ni kuyakataa Maandiko matakatifu. Wakati jambo hili lilipofanywa, lilibadilishwa kutoka “Kanisa kwa kuzaliwa” likawa “kanisa kwa mafundisho ya sharti na kanuni za imani.” Si *kanisa*, hebu niombe msamaha; loji! Unazaliwa katika Kanisa, lakini unajunga na loji. Si kanisa la Kibatisti, kanisa la Methodisti, kanisa la Kipentekoste. Ni loji la Kibatisti, loji ya Kipentekoste, na loji ya Kimethodisti, unajunga nazo. Huwezi kujiunga na Kanisa. Hakuna kitu kama hicho. Unazaliwa ndani Yake. Nikodemo aliambiwa jambo hilo. Kwa hiyo mnaona mahali mlipo? Loo, jamani!

<sup>179</sup> Hiyo ndiyo sababu mimi ninayapinga. Siwapingi watu walio ndani yake; mfumo ambaao ninaupinga. Maana hawawezi... Mmoja wa hao wazee ama cho chote kile, moja ya makanisa hayo yanahubiri kitu kilicho katika Biblia kinachopingana na fundisho hilo, mkataba walio nao katika kanisa hilo, anafukuzwa moja kwa moja namna hiyo. Naam, bwana. Wengine wao ni wabaya sana hatia hawataruhusu ufufuo uje kwenye kanisa lingine isipokuwa iwe ni mmoja wa watu wao wenyewe. Jamani, wako ninii mno...

<sup>180</sup> Mtu fulani wakati mmoja alikuwa anaenda kumpa mhubiri... Papa hapa katika nchi hii, maskini mhubiri mmoja mzee aliyesimama hapa barabarani, akilia na kuwasihii watu watubu, na kusema, “Njoni, mkampokee Kristo, mkajazwe na Roho Mtakatifu,” na mambo kama hayo. Na mtu fulani kutoka kwenye madhehebu ya Kipentekoste alikuja na kumpa mtu fulani dola moja mkononi mwake, na ilimbidi kutubu kwa maana ati alifanya uzinzi dhidi ya kanisa lake. Ati kunena kuhusu Katoliki! Hiyo ni kweli. Na mnajua ninalozungumzia, pia; ama kanisa hili linajua, hata hivyo. Vema.

<sup>181</sup> Kufanya hivi, kukataa Maandiko, wakati jambo hili linapofanywa, lilibadilika basi unapoongeza fundisho la sharti na kujiunga na madhehebu, moja kwa moja umekubali fundisho lako la kwanza la sharti, maana si la Kimaandiko, kwa hiyo ni jambo lililoongezwa. Ni fundisho la sharti, ni kitu kilichoongezwa “kuchukua mahali pa,” ni kuchukua mahali pa kuzaliwa. Unapokubali madhehebu, umeongeza mafundisho ya sharti. Vema. Wakati hili linapofanywa, basi linabadilika kutoka “Kanisa kwa kuzaliwa” kuwa “loji kwa fundisho la sharti ama kanuni ya imani.” Kwa kuwa, unaona, lenyewe lilivyo ni fundisho la sharti, kwa kutokuwa la Kimaandiko.

<sup>182</sup> Sasa, Yesu kamwe hakusema, “Enendeni ulimwenguni kote na mkafanye madhehebu, nendeni mkawaunganishe watu pamoja.” Yeye alisema, “Enendeni mkafanye wanafunzi.”

Mnaanimi jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina”—Mh.] Amina. Kwa hiyo, unaona, kwa jumla mko nje.

<sup>183</sup> Sikilizeni, angalieni hapa. Hebu na tulifunge kwenye jambo lingine hapa, tushindilie kitu fulani ndani wakati uu huu. Ni wangapi walio na kamusi ya Kiyunani, ile Emphatic Diaglott kutoka kwenye maandiko ya kale ya mkono, Kiyunani? Vema. Isomeni, mchukueni mwanachuoni ye yote mnayetaka. Nendeni kwenye maktaba na mchukue kamusi hiyo, kamusi ya Kiyunani. Someni Ufunuo 17, na mtakaposoma hapo, Tafsiri ya King James hapa inasema, na hivi, “Yeye akanichukua katika Roho; nikaona mwanamke ameketi juu ya mnyama mwenye mavazi mekundu sana, mwenye kuja majina ya—ya makufuru.” Sasa, hivyo ndivyo ile ya King James ilivyosema. Lakini tafsiri ya asili ilisema:

...akanichukua                   katika                   Roho...nikaona  
mwanamke...mwenye kuja majina ya kukufuru...

<sup>184</sup> Kuna tofauti kubwa sana kati ya “majina ya makufuru” na “majina ya kukufuru.” Sasa angalia. Sote tunafahamu na kujua ya kwamba hilo lilikuwa ni kanisa la Kirumi likiketi kwenye milima saba, likitawala nguvu za ulimwengu. Nalo liliitwa “kahaba,” nalo lilikuwa ni “mama wa makahaba.” Angalia! Kahaba ni nini? Inaweza kuwa ni mwanamume? Haina budi kuwa ni mwanamke. Kwa hiyo kama ni mwanamke, haina budi kuwa ni kanisa; lilikuwa ni mama wa makahaba, sawasawa na mama yao alivyokuwa. Pia angalia, tazama, “Ndani yake!” Hebu hilo likolee ndani. “Ndani yake kulikuwako na majina ya makufuru.” Ni nini? Sasa, wahudumu hapa na walio kwenye kanda, hebu na tutulie. Majina hayo ya makufuru ni yapi? Methodisti, Batisti, Presbiteri, Luteri, Pentekoste, kadhalika. Majina ya makufuru, kwa sababu ni madhehebu, ukahaba kwa Mungu, kama tu hilo lilivyokuwa.

<sup>185</sup> Nao, katika makundi hayo, watu hao husema, “Mbona, yeye ni Mmethodisti, na anafanya *hivi*. Yeye ni Mperekoste, na anafanya *hivi*.” Yeye ni Mperekosteri na anafanya *hivi*. Wanafanya jambo lo lote kwenye orodha ya miadi, mnajua hivyo. Na ni kitu gani? Ni majina yanayopaswa kuwa kama Kristo na kuitwa kwa jina la Mkristo, na ni majina ya makufuru! Hayo si makanisa. Yanaitwa “kanisa” kimakosa. Ni maloji! Sasa mnaona ni kwa nini mimi ninapinga madhehebu, si watu? Ule mfumo wa madhehebu, unaona, majina ya makufuru (angalia) ya maloji, yanayoitwa makanisa kimakosa. Kanisa la Kimethodisti, kanisa la Kibatisti, kanisa la Kipresbiteri, kanisa la Kipentekoste, kanisa la Kiluteri, kanisa la United Brethren, hakuna kitu kama hicho. Hilo si la kimaandiko.

<sup>186</sup> Kuna Kanisa moja tu, wala huwezi kujiunga Nalo. Umezaliwa Humo. Umechaguliwa tangu zamani Kwake. Mwili wa kisiri wa Yesu Kristo... Mwili wa kisiri, hasa, wa Yesu Kristo hapa duniani, pamoja na Neno likidhihirishwa. Wana na binti

za Mungu, hao si wafuasi wa lo lote la hayo. “Tokeni kati yao,” Yeye alisema. Naam.

<sup>187</sup> Angalia, upesi sasa. Sitaki kuwachosha, lakini mkinipa tu dakika nyingine chache sasa, nitaenda upesi niwezavyo, lakini ninataka mwe na uhakika na mlipate, kusudi msilikose. Unaona?

<sup>188</sup> Kumbuka, mama Rumi, ndani yake mlionekana, amejaaj majina ya kukufulu, mama wa makahaba. Basi, kama wao ni makahaba, kahaba ni nini? Malaya ni nini? Ni sawasawa na kahaba. Ni mwanamke asiyekuwa mwaminifu kwa nadhiri yake ya ndoa. Na kanisa lo lote linalodai kuwa ni Kanisa la Kristo, na linakana Neno la Mungu, si aminifu kwa nadhiri yake ya ndoa! Ndipo linafanya uzinzi kwa kuongeza mafundisho ya sharti, ukahaba na ulimwengu na hekima yake, badala ya kumkubali Kristo na nguvu za kufufuka Kwake, za Roho Mtakatifu. Na ni mama wa makahaba ambaye amefanya jambo lile lile. Nyungu haiiti birika kwamba “ina grisi,” mwajua; unaona, ni kitu kile kile. Baadhi ya watu hawa wanaondoka kuwachecha Wakatoliki, wakati wao wenye ni wafuasi wa kitu kile kile. Yeye alikuwa ni mama wa ubatizo wa uongo katika maji. Ni mama wa ushuhuda wa uongo wa Roho Mtakatifu, nanyi mnaambatana naye vizuri sana. Sasa hebu tuone.

<sup>189</sup> “Je! hiyo ni kweli, Ndugu Branham?” Hebu tulieni kidogo tu.

<sup>190</sup> Mnaona, yeye ni mama wa majina ya makufuru, ya maloji ambayo watu wamejiunga nayo, na kusababisha shutuma, wanaishi vyo vyote, wanavaa suruali fupi, wanaweke waliokata nywele, waliojipodoa, wanaoimba katika kwaya, wanavuta sigara, wanafanya ushirika, kila namna ya uchafu wa ulimwengu, na ni jiwe la kujikwaa kwa asiyeamini. Hivi Timotheo hakunena habari zake, Roho Mtakatifu? Angalia. Unaona, yeye, Rumi, ni mama ya kila moja yao. Unaona? Mlifanya sawasawa kabisa katika madhehebu yenu na vile hilo lilivyofanya, mkaingiza mafundisho ya sharti badala ya Neno, kwa sababu kundi la watu liliketi pamoja, wazee na maaskofu na kadhalika walisema lilipaswa kuwa *hivi*, na hiyo ndivyo ilivyotendeka hasa huko Rumi. Na unajaribu kuninii, ndugu yangu mchungaji, kubali Neno lote la Mungu, na, angalia mahali utakakokwenda, utatolewa nje moja kwa moja! Sasa tutaona kama Mungu alikwambia ufanye hilo, ama hakukwambia, katika dakika chache. Unaona? Vema.

<sup>191</sup> Unaona, yeye ni mama wa kila moja, kwa sababu yeye alikuwa wa kwanza kuondoa maneno ya Maandiko na kuongeza mafundisho ya sharti, kwa kuwa alikataa manabii waliotiwa mafuta ambaao walikuwa na maisha yaliyothibitishwa, pamoja na Neno. Kuchukua watu wenye akili, werevu, Wafalme wa Kirumi, na kadhalika, ambaao walikuwa wamekubali Ukristo,

bali wanataka...kuukubali kwa njia yao wenyewe. Mnaona? Hiyo ni kweli. Wanautaka kwa njia yao wenyewe.

<sup>192</sup> Naamani alitaka kuondoa ukoma wake katika maji ya nchi yake mwenyewe, hakutaka maji yenyе matope ya Yordani. Lakini kama wakati wo wote ataondoa ukoma wake, ingembidi kutembea atoke aende huko katika matope hayo sawasawa tu kama vile nabii aliyomwambia. Unaona, Mungu hana upendeleo.

<sup>193</sup> Angalia, ye ye alikuwa ndiye madhehebu ya kwanza. Waangalie binti zake, walikuwa wamefanya jambo lile lile, waliiongeza kanuni za imani na mafundisho ya sharti badala ya Neno. Usiniambie; nionyeshe moja ya hayo ambayo hayako nje ya Neno. Nionyeshe mchungaji mmoja atakayekubali ile Kweli, hao ambao hawataku fukuza, labda uwe unapendwa sana na watu hivi kwamba, unajua wewe yabidi wakushikilie kwa sababu ya kupendwa kwako na watu ama cho chote kile. Ni vema.

<sup>194</sup> Sasa angalia katika Ufunuo 18, kwa dakika chache tu, kifungu kinachofuata, mlango unaofuata, baada ya Ufunuo 17 amekuchunguza na—na kuonyesha siri ya huyu Bi Babeli. Sura ya 17 ya Ufunuo inaeleza ya kwamba ye ye ni kanisa linalokaa juu ya milima saba, Mji wa Vatican, unaowatawala wafalme wote wa dunia (hiyo ndiyo kweli kabisa), na Marais pia, na kadhalika. A-ha. Kwa hiyo, lakini yuko pale, limeushikilia utajiri wa ulimwengu mkononi mwake. Hiyo ni kweli kabisa. “Ni nani anayeweza kufanya vita naye?” Hiyo ni kweli. Sote tunajua jambo hilo. Lakini kwa nini wewe ujunge na kitu kinachomhusu ye ye? Sasa angalia katika mlango wa 18, mlango unaofuata tu mara baada ya siri yake kuelezweta. “Anaketi katika hekalu la Mungu.” Sasa, hapa, ninii . . .

<sup>195</sup> Zella Braitman, hivi uko hapa usiku wa leo, Zella? Alililetä, liko chumbani mle sasa, *Mgeni Wetu wa Jumapili*, lile gazeti la Katoliki. Na gazeti hilo la Katoliki lilikuwa likimjibu mhudumu. Kasema, “Je, ulisema, ya kwamba ninii . . . Katika tarakimu za Kirumi juu ya Vatican, ama kwenye kiti cha enzi cha Papa, imeandikwa, ‘Vicarivs Filii Dei,’ ambalo linamaanisha, kwamba katika dayosisi ya Katoliki pale, ya kwamba hiyo ni na—namba ya yule mnyama wa Ufunuo?”

<sup>196</sup> “Mbona,” ye ye akasema, “bila shaka, limeandikwa. Kweli kabisa limeandikwa, hesabu yake kweli ni mia sita sitini na sita. Ni kweli kabisa.” Na dayosisi ya Kirumi inakiri jambo hilo, kwamba hiyo ni kweli. Lakini wanajitetea hivi, wao ni werevu, wamejaa hekima, kasema, “Lakini, unajua, jina lako katika lugha fulani huenda hesabu yake ikawa jambo lilo hilo.”

<sup>197</sup> Mtu huyu akasema, “Langu, karibu ni jambo lille lile katika lugha fulani.” Akaandika herufi zake. Kasema, “Unaona, mimi ninakaribia mia sita na sitini na sita, pia.” Kasema,

“Kumekuwa na mamia yao.” Kasema, “Kila wakati jambo lo lote linapoinuka, mtu fulani ana mia sita sitini na sita.” Halafu akasema, “Kasisi, je! ulijua ya kwamba katika lugha fulani jina lako mwenyewe huenda likamaanisha herufi za mpinga Kristo?” Kasema, “Mbona mnaangalia mambo kama hayo?” Angalia hekima hiyo.

<sup>198</sup> Lakini Roho Mtakatifu anajua zaidi. Angalia. Hilo huenda likawa, jina langu linaweza kumaanisha mia sita sitini na sita, lakini mimi sitimizi sifa hizo nyingine. Mimi siketi juu ya mlima. Sisemi mambo *haya*. Mimi si liwali, unaona. Hiyo ni kweli. Huyo ndiye Yeye anayenena habari zake. Kwa hiyo hekima yako ya kilimwengu haifiki po pote, bwana, hiyo ni kweli, kwenye Uwepo wa Roho Mtakatifu. Mimi sitimizi hayo mengine, lakini yeye anayatimiza. “Akiketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake yeye ni Mungu na anakalia milima saba.” Mimi sikalii milima saba, hata kama linamaanisha mia sita sitini na sita. Sitimizi hayo mengine, lakini yeye anayatimiza. Unaona, haya basi. Unaona? Kwa hiyo wale wanaomtegemea Roho Mtakatifu, “Msifikiri-fikiri yale mtakayosema, kwa kuwa si ninyi msemao; ni Baba.”

<sup>199</sup> Kwa hiyo hekima yenu na kuzaliwa kwenu kunakotoka Juu kunawezaje kulinganishwa na mambo haya hapa duniani, hawa—hawa wachawi wakuu ndani yake? Mbona, wanajua kila kichochoro na kona. Musa angwezaje kusimama ambapo alifuata Amri za Mungu, kutupa fimbo yake chini na ikageuka kuwa nyoka, na hawa hapa wachawi wanakuja na kufanya jambo lile lile? Lakini Musa alisimama kimya, akijua alikuwa amekwisha tii Neno la Mungu, na ndipo nyoka wake akawala wale wengine. Unaona? Kwa hiyo wakati umetii na unaninii... Yeye angefanya nini wakati alipowaongoza kwenye nchi ya ahadi, na hapo palikuwapo na Bahari Nyekundu imewazingira, lakini njia ya Mungu ilipasua moja kwa moja kupitia humo. Amina. Kasema, “Simameni kimya, mkauone Utukufu wa Mungu!”

<sup>200</sup> Wakati jambo liko kwenye njia ya wajibu wa kazi, wa kuti Neno, simama hapo uone likifunguka. Amina. Nina umri wa miaka hamsini na mitatu, nimekuwa nikimtumikia Yeye kwa yapata miaka thelathini na mitatu, laiti ningalikuwa na miaka milioni kumi ya kumtumikia. Mimi kamwe sijawahi kumwona akishindwa umbali huu, Neno Lake linapofuatwa. Hiyo ni kweli.

<sup>201</sup> Sasa angalia, mara baada ya dhambi yake, siri zake zilifunuliwa. Tumefahamu hilo muda mrefu uliopita, tunalifahamu hilo.

<sup>202</sup> Sasa mlango unaofuata, angalia Ufunuo 18. Hebu niufungue kwa dakika moja tu. Ingefaa, halitatuchukua zaidi ya dakika chache, na huenda likamaanisha kitu fulani kidogo kwako. Ninatumaini litafanya hivyo.

<sup>203</sup> Sasa tunaona hapa, katika mlango wa 17, kifungu cha 5.

...katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, LA SIRI, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.

Basi angalia.

*Nami nikamwona yule mwanamke (kanisa) amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu: . . . nilipomwona nikastaajabu ajabu kuu.*

<sup>204</sup> Unaona, alipomwona, alikuwa ni kitu kizuri cha kupendeza sana. Naye alikuwa ni mama wa makahaba, dini ya makahaba, madhehebu, ndivyo hasa alivyofanya, unaona, maana waliingiza mafundisho ya sharti kama tu vile alivyofanya yeye. Sasa angalia, angalia kwenye Ufunuo sasa, huo ni mlango wa 17, inaishia kwa kifungu cha 18. Sasa angalia.

*Baada ya mambo haya, baada ya siri yake kuvumbuliwa, baada ya mambo haya nalionna malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; . . .*

<sup>205</sup> Sasa, huyu hapa mjumbe mwingine anashuka, mlango unaofuata, siri yake iligunduliwa. Basi, huku sasa ni kugunduliwa kwa siri yake na siri ya watoto wake. Unaona, tunafahamu sasa ni kitu gani hasa kilichomfanya kuwa kahaba: ni kwa sababu alifanya usinzi dhidi ya Neno la Mungu. Na jambo hilo ndilo lililomfanya madhehebu. Hangedumu kuwa kanisa la Biblia na akubali kitu hicho. Na wala madhehebu yo yote yasiyochukua kila Neno Lake (jinsi lilivyoandikwa) hayawezi kamwe kuwa kanisa la Biblia. Wala hakuna hata moja la hayo lililo namna hiyo, ambalo ninajua jambo lo lote kulihu, hata moja. Kwa hiyo hapo, unaona, mara linapofanya madhehebu vitu anavyofanya, (kwa Maandiko na kwa ushuhuda pia) linakufa papo hapo, linakubali mafundisho ya sharti. Sasa angalia, sasa hilo ndilo lililotukia.

<sup>206</sup> Mungu alituma, katika mlango huu wa 18, malaika mwenye nguvu, baada ya siri hiyo kujulikana, malaika mwenye nguvu, ama, mjambe. Angalia hapa.

*Baada ya mambo haya nalionna malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake.*

*Akalia kwa sauti kuu, . . . Umeanguka, umeanguka Babeli (machafuko) ule mkuu unaanguka, umekuwa maskani ya mashetani, . . . ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza; . . . ndege mchafu mwenye kuchukiza;*

*Kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi*

*wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata  
mali kwa nguvu za kiburi chake.*

<sup>207</sup> Angalia, mara baada ya siri yake kujulikana, kwamba alikuwa ni nani, alikuwa nini, binti zake walikuwa nani, siri imegunduliwa, basi Mungu alimtuma malaika, mjumbe (kufanya nini?) kuwaita watoke. “Tokeni!” Ujumbe wa Wakati huu!

. . . *Tokeni kwake, enyi watu wangu, msikashiriki  
mapigo yake, wala msipokee mapigo yake . . .*

Yeye atamlaani. Angalia.

<sup>208</sup> Tokeni kwake! Mungu alituma wengi . . . malaika mkuu, ama, mjumbe. Na Nuru yake haikuwa kwenye maficho, iliangaaza duniani kote. Tokeni kwake! Nini? Yeye, na dada zake, pia. Kuiangaza nchi, na kuwaita watu Wake watoke kwake. Sasa, mnajua jambo hilo ni Kweli. Mjumbe fulani alitumwa kutoka Mbinguni, kuwaita watu wa Mungu watoke Babeli. Na Nuru Yake ikaangaza nchi, Roho Mtakatifu aliye mkuu.

<sup>209</sup> Angalia, Biblia ilisema, “Yeye ni ngome, na ameshika ndege wenye kuchukiza, wachafu.” Si tai, sasa, la, la, la, la. Koho, “Ndege wachafu, wenye kuchukiza,” hao ndio aliovatia kwenye ngome kumzunguka. Yeye ni ngome iliyojaa hao, ngome yote imeja. Imeja nini? “Majina ya makufuru,” kinyume cha Maandiko, II Timotheo 3 ilisema, Roho Mtakatifu akinena, “Katika nyakati za mwisho watajitenga na Imani na kusikiliza roho zidanganyazo.” Pia yalisema, Roho Mtakatifu alisema ya kwamba “Katika siku za mwisho watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wenye kuchukiza (‘Mungu atukuzwe, wewe ni wetu, la sivyo kama jina lako halimo kwenye kitabu chetu, umepotea’). Wenye kuchukiza! Wachafu!” Natumaini mimi sisononeshi, natumaini ninafanya lililo jema. Ndege wachafu, wenye kuchukiza, amewaweka kwenye ngome.

<sup>210</sup> Kumbukeni, Mungu ni tai. Yeye alijiita tai. Kisha akamwita Yakobo tai. Nasi ni vifaranga Vyake vy a tai. Amina. Aliwaita manabii wake “tai.” Naye malaika huyu alishuka kuja kufichua na kuwaita watoke!

<sup>211</sup> Ni kama ule ujumbe wangu mdogo juu ya *Tai Anacharakisha Kiota Chake*. Maskini kifaranga huyo wa tai daima alikuwa akimfuata maskini yule kuku kila mahali katika ule uwanja wa ghala wakati wote, akifanya mlion wa kuku kila mahali, lakini hangeweza kula vile vitu alivyokuwa navyo, tafrija, na wanawake waliojipodoa, waliokata nywele zao, na vikaptura. Asingeweza kufanya hivyo. Lakini hakujua jambo lingine lo lote ila mlion wa maskini yule kuku mzee. Lakini siku moja mama tai alimwona. Akalia kwa sauti kuu, akimwita atoke, kasema, “Mwanangu, wewe si mmoja wao. Toka kwake!”

Kasema, “Mama, nifanyeje?”

<sup>212</sup> Kasema, "Pigapiga mabawa yako na uanze." Mruko wa kwanza, akapiga kizingiti, moja kwa moja katikati ya madhehebu. Kasema, "Mwanangu, itakubidi uje juu zaidi ya hapo la sivyo siwezi kukushika. Huna budi kuondoa miguu yako ardhini." Yuaenda kumchukua apae juu. Yeye akakuta kwamba angeweza kuruka. Mama tai akaja kumwita atoke. Hiyo ni kweli.

<sup>213</sup> Lakini huyu Mama Babeli alikuwa amejishikia kundi la kuku, vifaranga warembo, waliojipodoa, waliokata nywele zao, waliojiita "Wakristo." Ana ngome iliyojaa hao. Ninyi wahubiri mnaosimama mimbarani na kuwaachia hao wanawake wafanye hivyo, hamna aibu, kuyafanya madhehebu yenu yawe na watu wengi zaidi. Mungu atawataka hilo mkononi mwenu. Tokeni kwake! "Kondoo wangu wanaaisikia Sauti Yangu." Ngome ya watu wenyе kuchukiza, wakaidi, wenyе kujivuna, wanaopenda anasa kuliko kumpenda Mungu, ambaо wanaona heri kuwa kama ulimwengu kuliko kuwa kama Kristo. Unapomwona mwanamke mwenye vipodozi vingi sana, inaonyesha yeye ni mtupu ndani. Yeye huko ndani ni mdanganyifu. Hiyo ni kweli kabisa. Kama mwanamke... Nilimwona mmoja hivi majuzi, mwenye nywele za kijani kibichi, hiyo ni kweli, takataka hizo zote za kijani kibichi machoni mwake.

<sup>214</sup> Sasa, kama wewe—kama—kama hukuwa na nywele zo zote, na—na ultaka kuvaan nywele, ingekuwa ni sawa, lakini, vaa zile zinazoonekana kama za kibinadamu. Na endapo hukuwa na kucha zo zote, na—na ultaka kupata makucha machache, usinunue yale yanayofanana na maganda ya kunde, nunua—nunua kucha halisi. Kama huna yo yote ya mambo haya, ni sawa. Kama huna meno yo yote, jinunulie kama wanawatengenezeeni, nunueni. Lakini using'oe meno uliyopewa na Mungu ati kwa sababu tu yamepinda kidogo, nayo ni meno mazuri, kusudi ununue mengine. Usitie nywele zako rangi, ama cho chote kile, na kuonekana kama kitu kilichotoka kwenye matope mahali fulani. Usizitie rangi! Kama hazina rangi, na unataka kujitengenezea uonekane kana kwamba zina rangi, ni sawa, nadhani. Lakini usijifanye uonekane kama Yezebeli, kama ghala mahali fulani linalopakwa rangi.

<sup>215</sup> Nanyi ndugu wa Kipentekoste, mnaowaacha wanawake hao wakate nywele zao, wakati Biblia ilisema huo ni utukufu wake! Na hata si kawaida kwake kuomba wakati nywele zake ziko hivyo. Na hata hivyo unamruhusu apande mimbarani na kuhubiri Injili, kuimba katika kwenye, kufundisha shule ya Jumapili. Hamna aibu! Mwapaswa kujionea aibu. Ni kwa nini mimi ninapinga madhehebu? Mnadhani ningaliweza kamwe kushughulikia kitu kama hicho? Ninajua ni kwa nini unafanya jambo hilo, ndugu. Unajua ukweli, lakini kama ungefundisha dhidi ya jambo hilo, ungepelekwa makao makuu,

nao watakutenga. Mungu atukuzwe kwa ujasiri wako endapo utafanya hivyo. Hiyo ni kweli. Mungu atakuheshimu.

<sup>216</sup> Malaika huyu alisema nini? "Tokeni kwake!" Naam, bwana. Malaika huyu alikuja duniani, naye alikuja kuleta Nuru, naye aliangaza Nuru kote ulimwenguni. Alikuwa malaika mwenye nguvu. Naye alikuja kutangaza ujumbe wa "Tokeni Babeli! Msiguse vitu vyake vichafu!"

<sup>217</sup> Ana ngome nzima iliyojaa hao, kasema, "Ni ngome ya kila ndege achukizaye." Naam, ana ngome iliyojaa hao sasa, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, ama maloji. Ana kundi zima lililowekwa kizimbani sasa, wote wanaungana. Amekuwa ngome, vema, iliyojaa ndege wenye kuchukiza. Hiyo ni kweli. Jaribu kuzungumza na mmoja wakati mmoja, hebu jaribu tu hilo, loo, ni mwerevu kwa mambo ya ulimwengu, lakini hajui mengi zaidi kuhusu Mungu kuliko sungura anavyojua juu ya viatu vya theluji. Hiyo ni kweli. Ni ninii tu, hivyo ndivyo ilivyo hasa, unaona, yote tu wanayojuu ni hekima kidogo ya wao kuweza kuingiza *hiki* na *kile* na kufanya lile. Lakini inapokuja kwenye kumjua Yeye? A-ha! Naam, ameshikwa kwenye ngome yake na mafundisho yake ya sharti. Makanisa ya Kiprotestanti yalianza vile vile, yakawa binti zake, yalisababisha jambo hili kwa kukana Neno la Mungu. Hivyo ndivyo linafanya. Linakana Neno. Na wakati unapokubali jambo lingine badala ya Neno, unalikana mwenyewe. Na wakati unapojiunga na moja la hayo, wewe pia umelikana Neno. Mungu hataki uwe hivyo, hakuna mahali pake katika Maandiko.

<sup>218</sup> Angalia, huyu ni malaika wa Nuru, kumbukeni, malaika wa mwisho, ni malaika katika wakati wa kanisa wa Laodikia. Ni mjumbe wa Laodikia, huyo, ni wa mwisho, kwa kuwa mlango unaofuata tu ni mlango wa 19, ambao ni kuja kwa Bibi-Arusi. Na huyu ni nanii, katika Maandiko, ni malaika wa mwisho aliyejukua kuleta Nuru kabla ya kuja kwa Bibi-Arusi kwenda kumlaki Kristo. Ulikuwa ni Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati huo. Mjumbe wa Wakati wa Kanisa la Laodikia alikuwa nini? Akiwaita watoke Babeli! Angalia! Makanisa yameshikwa kwenye ngome yake na ninii yake, na mafundisho yake ya sharti, wakikana Neno na kukubali mafundisho ya sharti. Huyu ni Malaika wa Nuru kwa kanisa la Laodikia lililokuwa limemkataa Kristo na Neno Lake, kuchukua fundisho la sharti, na lilikuwa limemweka Yeye nje. Naye alisimama mlangoni, akibisha, akijaribu kuingia. Unaona hilo? Wakati wa kanisa ulikuwa umemkataa Kristo, na Kristo ni Neno, nao walikuwa wamelikataa, Naye alikuwa nje. Ndio wakati pekee wa kanisa ambapo Kristo yuko nje, akibisha, akijaribu kuingia. Na Ujumbe wa malaika huyu, mjumbe alikuja kutoka kwa Mungu, alikuwa akirudisha mwangwi Ujumbe wake duniani, wa "Tokeni Babeli! Tokeni kwenye madhehebu!" Roho Mtakatifu leo, dhihirisho la Roho Mtakatifu ni yule malaika akijaribu kuwarudisha watu

kwenye Neno, maana Roho Mtakatifu atathibitisha tu Neno. Hawezi kuthibitisha mafundisho ya sharti, hamna uhai ndani yao. Yeye ni Uzima. Angalia, Wakati wa Kanisa la Laodikia ulikuwa umemkataa Yeye, ulimkataa Yeye, nao wakamtupa nje.

<sup>219</sup> Angalia, malaika huyu ndiye mjumbe wa mwisho kabla ya kuja kwa Kristo katika mlango wa 19 wa Ufunuo. Sauti ya huyo mjumbe! Kama tukiangalia, wakati alipotoa Sauti yake duniani, kulikuwako na Sauti iliyorudisha mwangwi Mbinguni tena. Kifungu cha 4, kama mkitaka kusoma jambo hilo. Vema, kifungu cha 4, mlango wa 19. Huyu mjumbe duniani alikuwa ameegemea kwa Mungu sana hivi kwamba, wakati alipoutangaza duniani, Mungu alirudisha mwangwi jambo lile lile kutoka Mbinguni. Fasiri ya kifungu hicho cha 4 ni nini? Ina maanisha nini? Sauti ya Mungu ikinena na watu wake waliochaguliwa tangu zamani, ikisema, “Tokeni kwake!” Vile vile hasa ile Sauti ilivyokuwa! Alikuwa ana watu kila mahali, kote Babeli. “Tokeni kwake, msishiriki dhambi zake,” naam, bwana, kutoka kwenye hayo mafundisho ya sharti na kanuni za imani, kuingia kwenye Neno lililofanywa Roho na Uzima. Amina.

<sup>220</sup> Angalia, mlango wa 19 ndio unaofuata, “Baada ya mambo haya.” Je! mlitambua hapa katika mlango wa 19, “Baada ya mambo haya”? Ati uangalie nini? Baada ya kitu gani? Baada ya ule Ujumbe wa “Tokeni kwake!” “Baada ya mambo haya,” angalia, “ni makelele ya watakatifu ambao ni Bibi-arusi, pamoja na Bwana Arusi, wakienda kwenye Karamu ya Arusi ya Mwana-Kondoo.” Tumekaribia jinsi gani basi, ndugu? Wito wa mwisho ni nini? Tokeni Babeli!

<sup>221</sup> Sasa, ndugu zangu, hiyo ndiyo sababu mimi ninayapinga. Si ya kimaandiko. Si kitu cha kweli. Kimethibitishwa kuwa ni cha uongo. Mungu hayumo ndani yake, Yeye kamwe hajapata kuwa ndani yake, kamwe hatakuwa. Sasa, Mimi sisemi ya kwamba hakuna watu katika madhehebu haya, humo ndimo kanisa lilimotolewa. Lakini, mradi tu unakaa kwenye utaratibu huo, wewe ni sehemu yake.

<sup>222</sup> Kama nikikaa Marekani, mimi ni Mmarekani. Mradi tu mimi ni mwenyeji ama raia wa Marekani hii, mimi ni sehemu yake. Kama nikienda Ujerumani na nikane uanachama wangu hapa, ama uraiya wangu, nichukue uraia Ujerumani, mimi si Mwamerika tena, mimi ni Mjerumani. Na kama nikienda Japani ama ko kote kule, Urusi, ninakuwa raia wa huko.

<sup>223</sup> Na wakati unapojuunga na shirika—shirika fulani na unakuwa raiya wa shirika hilo, unaonyesha kwamba wewe ni nani. Na katika siku hizi za mwisho, Mungu anawaita watu watoke kwake. Biblia ilisema hivyo, “Tokeni kwake, msishirikiane naye, nami nitawapokea. Msiguse vitu vyake vichafu, mnaona, nami nitawapokea. Nanyi mtakuwa wana na binti Zangu, Nami nitakuwa Mungu kwenu.” Unaona?

<sup>224</sup> Hiyo ndiyo sababu nimenena dhidi ya kanisa, lo—loji. Siwezi kuliita kanisa. Kuna Kanisa moja tu, hilo ni Kanisa la Mwili wa Kristo. Lakini loji hizi zinazoitwa “kanisa,” Biblia yangu inaniambia ya kwamba hizo ni majina ya makufuru, yote hayo, madhehebu yote. Yanakufuru nini? *Kukufuru* ni “kuwa kinyume cha,” au “kunena dhidi ya.” Mungu anaposema “njoo uzaliwe,” na wao wanasema “njoo ukajiunge.” Unaona? Wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu unachukuliwa kimakosa kuwa ni mkate mwembamba katika kanisa Katoliki, kupeana mikono katika kanisa la Kiprotestanti, na mwamsho katika kanisa la Kipentekoste, badala ya Utu wa Kristo ukiingia na jengo lote zima hilo la piramidi tulilokuwa nalo hivi majuzi.

<sup>225</sup> Ongeza kwenye imani yako, wema, na kadhalika, yote haya katika Petro wa Kwanza, ninii wa 1 . . . Petro wa Pili, ninaamini, mlango wa 1, mahali ambapo yote yanaongezwa kwenye imani yako, mambo yote haya, utauwa, na usafi, na utakatifu, na kila kitu, na ndipo unatiwa muhuri na Roho Mtakatifu.

<sup>226</sup> Lakini ni kama tu mtu fulani waliyeninii . . . watu wanadai kuwa na haya wakati hawana, kwa sababu wamefundishwa kimakosa. Wamethodisti hupata hisia ya ajabu, walikuwa wakipata hiyo, na kutetemeka kidogo, ama—ama kucheza katika Roho. Wapentekoste wananena kwa lugha, ama—ama wanafanya jambo fulani la mwamsho. Ninaamini mambo hayo, bila shaka, lakini mambo hayo bila haya mengine hayafai kitu.

<sup>227</sup> Kama nilivyosema hivi majuzi, ni kama tausi . . . ama ndege mweusi akijaribu kuva manyoya ya tausi, ama kipanga akijaribu kutumia manyoya ya hua. Hayakukua toka mwilini mwake kamwe, aliyashindilia kwenye mwili wake mwenyewe. Ni ya kuijiwekea, ni madhehebu. Lakini wakati Mungu anapoweka kitu cho chote ndani mle, ni cha asili. Unajifanya mwenyewe kusema, “Nilijiunga na kanisa jana usiku. Siwezi kwenda tena, siwezi kunywa tena, siwezi kufanya *hili*. Nilijiunga na kanisa.” Unaona, unajaribu kuweka manyoya ya tausi katika mzoga wako wa koho. Hiyo ni kweli. Unaona? Unaona? Huna budi kuzaliwa mara ya pili! Huna budi kumpokea Kristo. Na unapompokea Kristo, huwezi kumpokea Kristo bila kupokea Neno Lake, kwa sababu Yeye ni Neno. Na wakati unapokuwa na mfano wa utauwa, na unakana Hilo, basi ninashangaa. Unaona? Na bado unaweza kuwa mfuasi wa madhehebu yote utakayo na uwe na mfano wa utauwa, na bado hujampata.

<sup>228</sup> Sasa, haya basi, marafiki. Hilo hapo jambo lote. Mungu awabariki. Mungu awasaidie. Sisemi jambo hili kusudi niwe tofauti. Ninajieleza binafsi. Hii ikiwa ni siku ya mapatano ya kukomesha vita, mimi siwekeani sahihi mapatano ya amani na ninyi wahudumu, hata kidogo, nafikiri inawapasa mje mwekeane sahihi nami; si na mimi, lakini pamoja na Mungu, Neno. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Semeni yale Biblia inayosema, semeni vile Hiyo inavyolisema Hilo. Kwa

sababu Biblia ilisema, "Yeye atakayeondoa ama kuongeza kwake." Nawe unaona, madhehebu si ya kimaandiko, na wakati unapopokea fundisho la kwanza la sharti ni afadhali urudi nyuma kabisa, maana unavuka mstari pale pale. Unaporudi kwenye kuzaliwa upya, ndipo basi utatembea kuingia kwenye Maandiko.

<sup>229</sup> Na ukiingia katika madhehebu, wao wanasema, "Ninajua, hatuamini katika *Hili*. Maaskofu wetu katika kanisa letu wanafundisha sisi ni moja ya makanisa ya zamani sana. Hatufundishi ninii..." Sijali kitu gani wao hawafundishi. Kama Biblia inafundisha jambo hilo, Roho Mtakatifu aliye ndani yako atalishwa kwenye Neno. Haidhuru mtu ni mwerevu jinsi gani na jinsi anavyowenza kulielezea vinginevyo, wanaweza kulielezea vinginevyo. Kafiri anaweza kuchukua Biblia na kumwelezea Mungu vinginevyo kwako.

<sup>230</sup> Kwa hiyo, hakuna mtu aliye na haki ya kuhubiri Injili isipokuwa amekuwa, kama Musa, kule nyuma kwenye mchanga ule mtakatifu ambako yeye na Mungu peke yao walismama, mpaka mtu amezaliwa mara ya pili na anasimama pale uso kwa uso na Mungu, na anajua. Hakuna kafiri, hakuna saikolojia, hakuna kuelezea, hakuna msomi ulimwenguni anayeweza kuliondoa Hilo kwako. Ulikuwapo wakati lilipotukia! Naam, bwana. Unajua yaliyotukia.

<sup>231</sup> Halafu unasema, "Nilipata tukio la namna hiyo, nami nina roho juu yangu." Na kama inakana Neno kwa njia yo yote, una roho mbaya. Unasema, "Mi—mimi siwezi kukubali upuuzi kama Huu. Ninajua, lakini kanisa letu..." A-ha, huyo hapo roho mbaya. Hiyo hapo alama yako ya utambulisho. Kaini, umetiwa alama. Naam, bwana.

<sup>232</sup> Hawa alikana tu Neno moja dogo; si yote aliyosema Mungu, Neno moja dogo tu, na ilisababisha kila maumivu ya moyo na kuvunjika kwa moyo, na kifo, na dhambi, na vita, na mengine yote, kila kaburi, kila ambulanzi iliyopata kupiga honi, kila hospitali iliyojengwa kwa ajili ya wagonjwa. Kutilia shaka kwake kudogo Neno moja dogo la Mungu, kulisababisha yote haya. Naye alifukuzwa, wakati jambo hili halikupaswa kutendeka. Utaingiaje, ukitilia shaka Neno moja Lake? Unasema, "Ninajua linasema *Hivyo*, lakini Hilo linaninii..." Linamaanisha Hivyo tu!

<sup>233</sup> Sasa angalia. Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kitu fulani. Huwezi kuwa na hukumu isipokuwa uwe na sheria kwanza. Hapana budi kuwe na kitu fulani, huna budi kuvunja kitu fulani kusudi uhukumiwe. Unaona? Na tena hakuwezi kuwako na hukumu, sahihi, bila adhabu. Sasa, unaona, huwezi kuwa na sheria mjini inayosema "faini ya dola tano kwa kuvuka taa nyekundu," na sheria nyingine iseme "la, anaweza kuwa huru." Unaona, huwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo hakuwezi kuweko na amri mbili zinazofanya kazi kwa wakati mmoja. Na

kuna amri moja, Mungu mmoja, Kitabu kimoja, Kristo mmoja. Basi. Imani moja, tumaini moja. Hivyo tu. Hiyo ni Biblia, Kristo.

<sup>234</sup> Angalia sasa, katika hili, kama kuna jambo fulani linalopaswa kuongezwa kwenye Hili, halina budi kuongezwa na mwanadamu. Haliwezi kuwa zaidi ya . . .

<sup>235</sup> Na kama Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa, kama Katoliki linavyosema, basi atauhukumu kwa kanisa Katoliki lipi? Yako mengi; kuna moja, la Kirumi; moja, la Kiyunani; na, loo, yako ya aina mbalimbali. Atauhukumu kwa kanisa Katoliki lipi? Ama, labda atauhukumu kwa la Kiluteri? Vema, basi, na labda Yeye atauhukumu kwa la Kipresbiteri? Unaona? Atafanya nini? Hatauhukumu kwa kanisa. Atauhukumu kwa Neno Lake. Vema, basi, Yeye kamwe hajaninii . . .

<sup>236</sup> Unaona, Yeye hawezi kuweka kundi la watu, kama vile ono la dada majuzi usiku, Roho Mtakatifu akamwagwa, alipitia moja kwa moja kupitia kwenye sanduku lile. Hakika, hakuna kitu kinachomshikilia Huyo. Ni mtu binafsi. Ametolewa apate kulisafisha kanisa, lakini haliwezi kumshikilia. Hakuna madhehebu yanayoweza kulishikilia. Ni hivyo tu. Haiwezekani kamwe. Una kila kitu humo ndani yako, wala huwezi kumshikilia. Madhehebu hayawezi kumshikilia. Lakini mtu binafsi ndiye aliye na Roho Mtakatifu. Sasa angalia.

<sup>237</sup> Ndipo basi kama Mungu atauhukumu ulimwengu kwa Neno Lake, basi bila shaka amelilinda na kuliweka katika hali njema. Ama, kama lote limevurugwa kabisa, Yeye atala hukumu namna gani? Unaona? Haina budi iwe ni jambo fulani. Yeye kamwe hakusema, "Mtu awaye yote kupitia kwa kanisa." Alisema, "Mtu awaye yote atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Hili, ama kuongeza Neno moja Kwake, huyo ataondolewa (sehemu yake) kutoka kwenye Kitabu cha Uzima." Kwa hiyo, kwangu mimi, ni Mungu, Neno Lake na hukumu. Sasa, kama nikiamua na kulikubali Neno, na nione kwamba Kristo alikuwa kwa ajili yangu, basi nitaomba kwamba Uzima Wake uingie ndani yangu na kuniongoza. Na kama Uzima Wake ni Neno, Naye aliandika hilo Neno, Uzima Wake unawezaje kuwa ndani yangu, nami ninadai kuwa na Roho Mtakatifu, na ninaongeza fundisho la sharti badala ya Neno? Isingewezekana. Ninawezaje kuongeza madhehebu wakati Yeye anayapinga, na kuthibitisha jambo hilo, na kulionyesha kupitia kwenye historia, ya kwamba kila wakati wanapounda madhehebu wanakuwa, kiroho? Loo, wao wanaongeza wafuasi, hakika. Hiyo ni kweli. Wanaongeza wafuasi. Lakini, kiroho, hawaendi mahali po pote. Nionyeshe, niambie katika historia ambapo kanisa liliwahi kuninii . . . Baada ya kuunda madhehebu, lilituwa papo hapo, Roho Mtakatifu aliliacha. Hakuna miujiza na ishara tena, nalo ilienda moja kwa moja likaingia kwenye machafuko.

<sup>238</sup> Hilo ndilo lililotukia hasa kwa makanisa yetu ya Kipentekoste. Yalifanya yale hasa mama yao aliyofanya. Hapo

mwanzo, walitoka, watu walioyakataa madhehebu. Sasa, baadhi yenu ndugu mnaosikiliza kanda hii, baadhi yenu ninyi wazee, mnajua ya kwamba miaka kadhaa iliyopita, miaka arobaini, hamsini iliyopita, kama wangalizungumza nanyi juu ya madhehebu, mngalisema ilikuwa ni kukufuru. Lakini leo ninyi ni wafuasi wa kitu ambacho mlifikiri ni kukufuru. Ninyi wanawake mnaokata nywele zenu na kujipodoa uso, mama yako alipinga jambo hilo, maskini mtakatifu huyo m—mzuri wa kipentekoste. Ilikuaje kwenu? Paulo alisema, “Mlikuwa mkipiga mbio vizuri, ni kitu gani kiliwazuia?” Mnaona? Huko nyuma mlikuwa huru na upuuzi huo, lakini mlitaka kuwa kama hao wengine.

<sup>239</sup> Ndivyo hasa Samweli alivyo sema. Israeli walikuwa na Mfalme, na huyo alikuwa ni Mungu. Nao walisema, “Samweli, unazeeka. Tufanyie mfalme, tunataka kuwa kama walimwengu wengine. Tunataka kuwa kama mataifa mengine. Tunataka mfalme wa kutupeleka vitani, tunataka mfalme anayeweza kutupigania vita vyetu.” Na hilo lilimkasirisha Samweli.

<sup>240</sup> Akasema, “Je, nimeshachukua cho chote kutoka kwenu? Je! nimewahi kuchukua pesa zenu? Je! nimewahi kuwaomba maksai ama cho chote? Nimewahi kuwaomba cho chote?”

Wakasema, “La. Hujawahi kutuomba cho chote.”

<sup>241</sup> Ama anasema, “Nimewahi kunena neno lo lote katika Jina la Bwana ila lile tu lililotimia?” Hiyo ni kweli? Akasema, “Basi msimpokee huyo mfalme, kwa sababu litamaanisha machafuko kwenu?”

<sup>242</sup> Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani, enyi Maskani ya Branham. Mnakaribia karibu kukua kuwa maskani kubwa sasa. Ninaweza nisiwepo kwa muda kidogo. Huenda nikaenda mahali fulani. Ni vigumu kujua ambako Bwana ataniita; labda niondoke jukwaani, labda kurudi hudumani, labda Yeye anaweza akaniita kwenda jangwani. Sijui atakakoniita mpaka Yesu atakapokuja. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Je! nimepata kuwaomba kitu cho chote? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Nimewahi kuwaomba pesa? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Nimewahi kuwaambia jambo lo lote, kati ya maelfu ya mambo ambayo nimewaambia katika Jina la Bwana, bali, hayakutimia? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Basi kamwe msijiunge na madhehebu. Ni kinyume na Neno la Mungu. Tokeni kwake kama mko ndani yake, na mkatengewa na mpokee Neno la Bwana. Na tuinamishe vichwa vyetu.

<sup>243</sup> Mungu mkuu wa manabii, Mungu wa Ibrahim, Isaka, na wa Israeli, ongeza nguvu, Bwana, kwenye ujumbe huu mdogo uliokatwa ambaa ulikuwa moyoni mwangu kwa muda mrefu, upate kwenda kwa ndugu zangu. Wengi wa hao walio huko nje, Bwana, wana mawazo mabaya juu yangu. Wanafikiri ya kwamba ninataka kuwa tofauti. Wanafikiri

kwamba ninajaribu kuwa mjuvi. Wamewaambia watu ya kwamba ninawadanganya watu, hasa sana katika mafundisho kama ya *ubatizo wa maji* katika Jina la Bwana Yesu, na juu ya *uzao wa nyoka*, yule *kahaba mkuu*, na nyingi za hizo kanda ambazo zilisambazwa zikiwa hazina cho chote ila Ukweli mtupu usiogoshiwa. Nami nimewauliza baadhi yao, “Baadhi yenu njoni mnionyesha ambapo nimefanya dhambi, ama kutokuamini ama kufasiri Neno vibaya.” Wala hakuna hata mmoja wao amekuja. Ninakuomba, Baba, hebu jalia watu hawa wajue ya kwamba wanaikosa ile saa. Watangojea hata iwe wamechelewa sana, wasipokuwa waangalifu. Naomba wao, kila mmoja . . .

<sup>244</sup> Bwana, nina hakika ya jambo hili, moyo wangu ungevunjika kama Andiko hili halingekuwa dhahiri kwangu, wakati Wewe uliposema, “Wote alionipa Baba Yangu, watakuja. Kondoo wangu huisikia Sauti Yangu.” Basi, Bwana, nadhani Ufalme kweli ni sawasawa na ulivyosema Wewe, ninajua ni hivyo, ni kama mtu aliyechukua jarife naye akaenda ziwani, akalitupa jarife na kuvuta wa kila aina. Kulikuwako, hapana shaka, na samaki mwenye kula takataka, walikuwako kasa, buibui wa majini, nyoka, kila kitu kilichonaswa na jarife la Injili. Lakini hatimaye, baadaye, kamba wa maji baridi, samaki mtambaaaji akarudi majini tena, kasa akajiondoa, nyoka akatoa sauti na kurudi shimonii, kama mbwa kurudia matapiko yake ama nguruwe kwenye matope yake. Lakini kulikuwako na samaki halisi pale, Bwana. Nami nina faraja hii, ya kujua ya kwamba, hata kabla ya jarife kuwafunika, walikuwa samaki wakati huo. Walizaliwa samaki waliokusudiwa, Na vivyo hivyo na jarife la Injili linalowanasa kwenye ufufuo. Unajua walio Wako. Jambo pekee ambalo ninahusika nalo, Baba, nijuavyo mimi, ni kudumu mkweli kwenye Neno hili. Wewe Ndiwe unayeamua nani ni nani. Nami ninajua ya kwamba kama vile kasa asivyoweza kuwa samaki, vivyo hivyo na mwanamume ama mtu, aliye bubu kwa Injili, hawezi kufahamu Ukweli. Kwa maana Baba ameona jambo hili tangu zamani, Nawe umeahidi ya kwamba wote aliokupa watakuja.

<sup>245</sup> Baba wa Mbinguni, ninakuomba ya kwamba kila mtu anayeusikia Ujumbe huu mdogo, kwamba Nuru ambayo umehubiriwa kwayo, na ninavyowawazia moyoni mwangu binadamu wenzangu, watu ambao uliwafia Wewe. Na watu, wengine walio huko nje, Bwana, kama kwenye kundi la Kora, watu waaminifu, wanaoongozwa vibaya, wakiwa na chetezo kitakatifu mkononi mwao, lakini wakaangamia. Mbona, hata wasingeruhusu chetezo cha moto kiingie pamoja nao; mwana wa Haruni, Eliezeri, ilimbidi akiokote. Nao walitengeneza beramu ya madhababu kutoka kwenye mabirika hayo, ngao, kuonyesha, na kuwa kumbukumbu ya kitu hicho cha kuchukiza, ambapo Kora alijaribu kuunda kundi dhidi ya mjumbe wa Mungu. Na iwe mbali nasi, Bwana. Roho Mtakatifu na atulinde daima.

<sup>246</sup> Tunakushukuru, Bwana, ya kwamba kanisa letu dogo, madhababu hii ndogo takatifu. Miaka mingi iliyopita, miaka thelathini na kitu, nilipiga magoti kwenye bwawa hapa lililoaja majani na unyevu, nasi tukauweka wakfu uwanja huu kwa ajili Yako, jengo hili dogo. Na kule pembedi mwa maskani hii kuna lile ono. Hilo lilitimia barabara kabisa. Lingali pale. Hawatalibomoa, Bwana, wataninii tu . . . linachakaa, nao watalihifadhi tu kwa kuweka moja juu yake. Mungu, jalia ya kwamba Injili hii ya heri ilioandikwa katika kurasa hizi hapa, naomba isiliache kanisa hili dogo mpaka atakapokuja Kristo. Jalia kila mshiriki, kila mshiriki wa Mwili wa Kristo, wanakuja hapa kutoka kote nchini na kote ulimwenguni, naomba kila mmoja wao apokee Nuru, Injili, na atembee ndani Yake basi na kumpokea Kristo.

<sup>247</sup> Pia jalia kwamba liwe halisi sana kwamba Maneno Yake yatatimia, "Kazi nizifanyazo Mimi, wao nao watazifanya. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye alienipeleka, yuna Uzima wa Milele." Na Uzima wa Milele unapoingia, wanazaliwa kutoka Juu, na kazi zitokazo kwa Mungu zinajidhihirisha zenyewe, kwa maana ni Uzima ule ule uliokuwa ndani Yake. Hauwezi kufanya jambo lingine lo lote.

<sup>248</sup> Kwa hiyo, Baba, jalia kanisa hili lisiweke kikomo chao cha Milele juu ya msisimko, juu ya madhehebu, juu ya cho chote pungufu ya Kristo Mwenyewe akiishi ndani yao, akithibitisha Neno Lake kupitia kwao na ahadi Yake. Naomba, tokea mtoto mchanga sana aliye hapa usiku wa leo, mpaka mtu aliye mzee sana, wapokee ujuzi huu. Na jalia kila mwanamume ama mwanamke, mvulana kwa msichana, anayesikiliza kanda hii, jalia iwe hivyo kwao, Bwana, na uwape kujua ya kwamba mimi ninajaribu tu kuwaonya na kuwaita watoke, kwa kuwa saa hii imechelewa kuliko tunavyodhania.

<sup>249</sup> Nasi tunaona Babeli, mama wa kahaba, na binti zake wote malaya wakijikusanya pamoja. Mungu, tunatambua ya kwamba Maandiko yanasema ya kwamba magugu kutoka kwenye mashamba ya ngano yatafungwa kwanza, matitamatita. Nayo yamefungwa matita-matita, wakijiita wenyewe majina ya makufuru ambayo kweli si yao, wala si ya Kanisa, pia; hayo ni maloji, si makanisa. Kuna moja lao tu, Baba, na hilo ndilo Wewe alilofia.

<sup>250</sup> Pia naomba, Baba, tunapoyaona hayo yote yakifungwa matita-matita sasa kwa ajili ya moto wa atomiki hivi karibuni, naomba, Bwana, ya kwamba utajalia ngano ijae na iwe nzito. Tujalie, Bwana. Naomba tukue na kuangaza Nuru, na tuwe kama Yesu, "Nisipofanya mambo ambayo Mungu alinitaka nifanye, basi sina Uhai ndani Yangu. Lakini kama Mungu akinena na kuonyesha Uzima Wake, basi hilo linajitetea Lenyewe." Naomba utujalie, Bwana. Ninaukabidhi Ujumbe huu Kwako, na kwamba utaulinda, na kuwaleta makumi elfu,

Bwana, ama, watoto Wako wote waliochaguliwa tangu zamani kwa Injili. Katika Yesu Kristo, Ambaye ni Neno, katika Jina Lake naomba. Amina.

Nampenda, nampenda  
 Kwani alinipenda kwanza  
 Na kununua wokovu wangu  
 Mtini Kalvari.

<sup>251</sup> Nitauliza swalii. Ni wangapi usiku wa leo katika wasikilizaji wanaoonekana hapa, wa hili kanisa kubwa la watu, ama nyumba iliyojaa watu, hasa, katika mahali hapa pa kuabudia, wanaoamini kwa moyo wenu wote, maisha yenu yanaambatana na masharti (ninyi) ya Mungu na Biblia, nanyi mnaamini jambo hilo, kwa kuyaangalia maishani yenu wenyewe, na kuona vile Roho anavyotenda kazi ndani yenu, ya kwamba yanaamini kila Neno jinsi lilitivoandikwa, na kilitimiza? Mnaamini? Mungu awabariki. Na aweke Roho Wake daima juu yenu.

<sup>252</sup> Na kwa rafiki yangu kwenye kanda, laiti mngaliweza kuangalia hapa kwenye kusanyiko hili usiku wa leo, nadhani watu wasiopungua asilimia tisini waliniua mikono yao, kwamba wameamini na kuangalia Biblia, (si vile kanisa lisemavyo) vile Biblia inavyosema, (si vile loji inavyosema) vile Biblia inavyosema, nao wanaona Maisha ya Kristo yakiakiswa ndani Yake.

<sup>253</sup> Mnajua, zamani za kale kabla ya kuwa na viyeyusha madini, sonara alikuwa akipiga dhahabu kwa nyundo. Nadhani mmesikia habari hizo. Kabla ya kupelekwa kwa myeyushaji, waliipiga. Na dhahabu ni madini yaliyo mazito kuliko yote, ni nzito kuliko risasi. Na kwa hiyo nimefanya utafutaji madini kidogo, na unaweza kuchukua mchanga ufuoni katika majangwa, na kusugua mkono wako kwenye mchanga, na halafu (whoooshii) unapulizia namna hiyo, na mavumbi na kila kitu vitaruka, mawe, lakini dhahabu ni nzito sana inakaa pale. Ndipo wakati unapochukua dhahabu hiyo, imefingirishwa kwenye uchafu mwangi sana hata imeokota mwangi sana. Na katika miaka ya volkeno ilipokuwa inajikusanya, ilipata mashapo na kila kitu, mavi ya chuma na vitu vingine vilivyochanganyikana nayo. Mfua alikuwa akichukua bonge hili la dhahabu na kulifua na kuligeuza, na kulifua na kuligeuza, mpaka akaondoa uchafu wote kutoka kwake. Na je! unajua jinsi alitivojua ya kwamba ametoa uchafu wote? Aliweza kuona sura yake imeakisiwa ndani yake.

<sup>254</sup> Na hivyo ndivyo Mungu anavyolifanya Kanisa. Yeye anafua kila kanuni ya imani, kila madhehebu, kila fundisho la sharti la kujibunia, mpaka anapoona Maisha Yake Mwenyewe yameakisiwa ndani yako. "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini." Unaona? Kama kile kilichokusudiwa kwa Kanisa, Uhai uliokuwamo katika Kristo kama hauakisiwi ndani yako, usitulie, kama huna subira, nguvu, mambo haya yote, na kiasi,

na—na mambo mengine, na utauwa, na upendano wa ndugu, na mambo haya yote unayopaswa kuwa nayo. Haidhuru umefanya jambo gani, haidhuru umepiga kelele namna gani, umejiungu na makanisa mangapi, umejibandika manyoya mangapi, usifanye jambo hilo. Ngoja mpaka kweli toka moyoni mwako unaweza kusamehe, kutoka moyoni mwako, mpaka ndani ya moyo wako una upendano wa ndugu. Haidhuru kama watang'oa konzi moja la ndevu kutoka shavuni mwako, unaweza kugeuza shavu hilo lingine kwa utamu, unaona, mpaka nguvu hizo, haidhuru wanakwambia nini.

<sup>255</sup> Wakati walipoweka kipande cha kitambaa usoni Mwake na kumpiga kichwani, kasema, "Sasa, wananiambia ya kwamba Wewe ni Nabii." Sasa wakaondoa kile kitambaa ghafla kutoka Kwake, na mmoja ameshika fimbo, kasema, "Ni nani kati yetu aliyekupiga? Tabiri na utuambie, kwa maneno mengine, ndipo tutaamini kwamba Wewe ni Nabii." Hakufungua kinywa Chake kamwe.

<sup>256</sup> Unaposikia nabii akiinuka, aliye na majibu yote kwa kila kiinimacho unachoweza kuzusha, kumbuka, huyo si nabii. Leo hawana budi kujua kila kitu, kwamba utaumwa na jino siku gani na utaumwa na tumbo, na cho chote kile, na kukwambia habari zake zote. Hiyo si tabia ya Mungu wetu. Waangalie manabii, mwangalie Yesu.

<sup>257</sup> Mwangalie Paulo, wakati angaliweza kumpiga mtu upofu, na akamwachilia mfua shaba amfukuze nchini, "Nadhani amepoteza nguvu zake za kumtia upofu."

<sup>258</sup> Yesu, Ambaye aliweza kuwafufua wafu, na hata hivyo ilisema askari mlevi alimtemea mate usoni Mwake, na kumchuna na kumtemea mate na kung'oa ndevu Zake kutoka usoni Mwake, na kumpiga kichwani, wakati amefungwa tambaa, kasema, "Tabiri utwambie ni nani aliyekupiga." Wala hakufungua kinywa Chake.

<sup>259</sup> Usiwaangalie hawa wafanya viinimacho wote. Lakini kumbuka, wanazungumza tu, dola bandia inaonyesha tu ya kwamba kuna ilio halisi mahali fulani. Unapoona upuuzi huu wa kimadhehebu ukikua na kustawi, kama lilivyosema "uchumi utafanikiwa mikononi mwake," kumbukeni tu, kuna Kanisa dogo la Mungu mahali fulani, kweli limejazwa na Roho Mtakatifu, la kweli, linalopanda ngazi. Usiyaangalia madhehebu makubwa.

<sup>260</sup> Ni kanisa gani kubwa zaidi lililonenwa katika Biblia kuliko wakati wa kanisa la Efeso? Na wakati Paulo alipopita kati ya pwani za juu za Efeso, na akaja kwenye kanisa hili, lilikuwa na watu kumi na wawili. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Nao wote walikuwa ni watu wazuri, wakapaza sauti na wakawa na wakati mzuri sana, lakini hawakuwa wamempokea Roho Mtakatifu

bado. Paulo akasema, “Je! hamjampokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wakasema, “Mbona, hatukujua kulikuwako na Roho Mtakatifu.”

<sup>261</sup> Akasema, “Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?” Kama hilo halikuleta tofauti yo yote, aliliambia nini kanisa hilo hapo?

<sup>262</sup> Wao walisema “Tayari tumebatizwa na mmoja wa watu mashuhuri sana aliyewahi kusimama duniani, Yohana Mbaitaji, ambaye alimbatiza Bwana wetu. Je! kubatiza huko si kuzuri nya kutosha?”

<sup>263</sup> Akasema, “La, bwana. Hamna budi kubatizwa tena, maana ufalme umetiwa muhuri kwa jambo lingine lote.” Nao waliposikia haya... Kasema, “Yohana alibatiza tu kwa toba, si kwa ondoleo la dhambi, akisema ya kwamba mnapaswa kumwamini Yeye ajaye, yaani, Yesu.” Nao waliposikia jambo hili, walibatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Sawa, kweli kabisa. Waliyafuata Maandiko.

<sup>264</sup> Mnajua, katika kuwekwa wakfu asubuhi ya leo, Musa aliufuata mfano aliuona Mbinguni, na akapiga hema kuuwakilisha. Wakati Sulemani alipolijenga hekalu, yeye (alifanya nini?) aliufuata mfano ambao Musa, kwa hema, akiweka Maandiko sawasawa.

<sup>265</sup> Na wakati Mungu alipokuja kwenye Hekalu Lake kwa ajili ya siku za mwisho, Hekalu hili, Roho Mtakatifu, “mwili uliniwekea tayari,” Roho Mtakatifu alishuka kwenye Siku ya Pentekoste, ujumbe ulikuwa, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na wote watakaoitwa na Mungu Bwana wetu wamjie.” Kama ukitaka kumwita mhudumu wenu daktari, Daktari Simoni Petro aliandika maagizo, maagizo ya Milele. Hayo ndiyo yanayomponya mgonjwa.

<sup>266</sup> Mnawaachia baadhi ya hawa mabingwatapeli wauza madawa wakijaribu, kwa madhehebu, kuyajatimiza kwa njia nyingine, hiyo ndiyo sababu wana... Mwajua, kama huongezi ninii... ukiongeza mambo mengi sana kwenye hayo maagizo, huenda ukandinii... sumu nyingi kupita kiasi, huenda ukamuua mgonjwa wako. Kama usipoweka ya kutosha ndani yake, u-... si kwa dawa ya kiuasumu, kama usipofanya hivyo, haitamfaa kitu mgonjwa wako. Daktari wako anajua jinsi ya kuandika maagizo.

<sup>267</sup> Na Kristo, Roho Mtakatifu, Ndiye Mwenye Kuandika yale Maagizo, naye aliyaaandika. Usiyaongeze wala usiyapunguze, kunywa tu dawa jinsi ilivyoagizwa. Ndiyo tiba ya magonjwa yote. Mungu awabariki. Mnampenda? Amina.

Nampenda, na-...[Nafasi tupu kwenye  
kanda—Mh.]

Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>268</sup> Sasa wakati tunapouvumisha, sasa geukeni na kupeana mikono na jirani yako hapo. Loo, ye ye ni msafiri pia, apitaye.

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na . . . -kovu wangu  
Mtini Kalvari.

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Calvari.

Nampenda, (hebu natuuimbe sasa), nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>269</sup> Sasa na tuinamishe vichwa vyetu, tufunge macho yetu, tuinue mikono yetu na sauti zetu kwa Mungu sasa, ninapowakabidhi kwa mchungaji. Tuna furaha kuwa pamoja nanyi hapa. Sisi si madhehebu. Hatuna sheria ila upendo, hatuna kanuni ya imani ila Kristo, hatuna kitabu ila Biblia. Hatuna uanachama; ni ushirika tu kwa Damu ya Yesu Kristo inayotusafisha kutoka kwa kutokuamini kote.

<sup>270</sup> Vema, sote pamoja sasa. “Nampenda, nampenda.” Mungu awabariki. Mrudi mkatutembelee tena. “Kwani alinipenda . . .”

Vema, mchungaji. Mungu awabariki. “Na kununua . . . wangu.”



*KWA NINI NINACHUKIA DINI ZA KIMADHEHEBU* SWA62-1111E  
(Why I'm Against Organized Religion)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, 11 Novemba, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ultolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 2003 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2003 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)